Jumatatu Agosti 19, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581773

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



UKURASA 21

**ARTETA AKIONA KIVULI CHA MESSI KWA SAKA**

UKURASA WA 3

**Watiwa** mbaroni wakidaiwa kutaka kutapeli watawa, pembe za ndovu

UKURASA WA 3

**Asilimia** 85 ya Watanzania wanatumia vitochi - ripoti

UKURASA WA 16



**DC** anusa ufisadi mradi wa vyoo, maji katika zahanati za vijiji vinne

# Lissu: CHADEMA ijibu hoja za Mch. Msigwa

• **Ni** kuhusu matumizi ya mabilioni ya shilingi..

*Endelea Ukurasa 2*



Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu

## Ukinzani wa insulini mwilini tishio

• **Prof.** Janabi aonya wengi hawajui wanaishi na maradhi; katika kila watu 10, tisa wana tatizo... *Endelea Ukurasa 2*



### DALILI ZA TATIZO

1. Nguvu za kiume kupungua, kukosa hamu tendo la ndoa
2. Kiuno kuzidi inchi 40 (wanaume), inchi 35 kwa wanawake
3. Kuota vinyama au madoa meusi mwilini
4. Magoti na viungo kuuma, kuwaka moto
5. Mwili kuishiwa nguvu

## Rais Mwinyi aona fursa Tamasha la Kizimkazi

UKURASA 3

**MICHEZO** **AWESSU, MASHAKA MOTO MPYA SIMBA** UK.24

**MAONI,** UK.6




Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wakiwa pamoja wakati wa mkutano wao wa kawaida wa 44 uliofanyika mwishoni mwa wiki Harare, Zimbabwe. **PICHA: IKULU**

# Lissu: CHADEMA imjibu Msigwa

**Na Halfani Chusi**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema kuna haja uongozi wa chama chake kujibu hoja ya aliyekuwa Mjumbe wa Kamati Kuu, Mch. Peter Msigwa, kuhusu matumizi ya mabilioni ya shilingi.

Kutokana na rai hiyo ya Lissu, chama hicho kimejibu hoja hiyo ya Mch. Msigwa, kikidai mwanachama huyo mpya wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuibua kashfa dhidi ya CHADEMA ni kusaka umaarufu kisiasa na si vinginevyo.

Akihojiwa katika kipindi cha 'Medani za Siasa' cha Star Tv, Lissu alisema ni vyema ofisi ya Katibu Mkuu wa CHADEMA ikajibu hoja za Mch. Msigwa kwa kuwa si ngumu.

"Ninafikiri kitu cha kujiuliza hayo malalamiko yake yako sahihi kiasi gani na mimi nilisema hoja zake zijibiwe na mamlaka sahihi za chama, hoja si ngumu 'kivile', rekodi za pesa zipo, na haya mambo tunayazungumza kila siku," Lissu alisema.

Mkurugenzi wa Itikadi, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia suala hilo, alisema:

"Msigwa hana hoja yoyote inayostahili kujibiwa, kwa miaka mitano mfululizo tumepata hati safi za ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Msigwa akiwa mjumbe wa Kamati Kuu, alikuwa sehemu ya wajumbe wa Kamati Kuu ambako taarifa ya fedha hupelekwa.

"Pili, Msigwa anafanya propaganda za kisiasa na anatafuta umaarufu kupitia CHADEMA ili ajibiwe, hatuna huo muda. Kwa sasa tunajiandaa kwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

"Tatu, Msigwa hana hoja mpya kwani anazungumzia mambo ya... (alitaja jina la kiongozi wao aliyehama na kujiunga na CCM) ya mwaka 2019.

"Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) walichunguza na kukuta ni mambo ya uongo na ya kuchafua chama, ila anataka tujadili porojo hizo.

"Msigwa ajikite kukisemea chama chake kipya na awatafute familia yake wamuunge mkono, ili angalau awe na faida huko alikokwenda. Ila tunamshukuru kwa kuitangaza CHADEMA kwa wanachama wa CCM ambao hawaji kwenye mikutano yetu.

"Amekuwa mwenezi mzuri kwani kila siku haishi kuitaja CHADEMA. Wale mabalozi wazee huwa hawaji kabisa kwenye mikutano yetu ila sasa tunawafikia kupitia Msigwa."

Mrema pia alinukuliwa na chombo kimoja cha habari jana akisema ni vyema Msigwa akaweka hadharani ushahidi wa tuhuma anazoelekeza kwa chama hicho badala ya kuongea kwenye majukwaa ya kisiasa.

"Haiwezekani mtu akaenda kusema uongo huko hadharani, hana ushahidi kisha chama ndio kimsaidie ushahidi, aweke hadharani ushahidi kwani tunajua anafanya porojo za siasa," alisema na kuongeza:

"Mali zote zinazohamishika na zisizohamishika za chama zipo salama chini ya Bodi ya Wadhamini, ambayo ndio msimamizi mkuu wa mali hizo, na rejesta ya mali hukaguliwa na CAG kila mwaka," alisema Mrema.

Tangu Msigwa ajiunge na CCM Juni 30 mwaka huu, amekuwa akirusha tuhuma dhidi ya chama chake cha zamani - CHADEMA kwenye majukwaa ya kisiasa, akidai kuna ufisadi ndani ya chama hicho, akitoa mfano wa zaidi ya Sh. bilioni mbili zilizochangwa na wabunge wa CHADEMA mwaka 2015, akidai hazijulikani ziliko.

Pia alitaka CHADEMA kuweka wazi matumizi ya fedha zilizochangwa wakati wa Operesheni ya Join The Chain, ambazo zilikusanywa kwa njia ya benki na mtandaoni.

Katika mahojiano na Stars TV, Lissu alisema, "Mimi na Msigwa ni marafiki tangu mwaka 2006 kwa sababu tulikuwa tunapambania kitu kimoja.

"Amejiunga na kambi ya uadui, sina cha kuzungumza naye, sijui kama atanipigia, nimejisikia vibaya sana kwa sababu nimefanya naye kazi kwa miaka mingi."

hosplan

**TUNALETA HUDUMA ZA AFYA ZA KISASA NCHINI TANZANIA, KUTOKA INDIA.**

sarvodaya HEALTHCARE
hitech Sai HOSPITAL




- **Pata unafuu wa maumivu sugu ya mgongo kwa kutumia teknolojia ya kisasa**
- **Uchunguzi na matibabu ya kina, kutoka kwa Daktari bingwa wa uti wa mgongo kutoka India.**

Daktari wetu bingwa wa uti wa mgongo, **Dk. Anchit Uppal**, kutoka Hospitali ya Sarvodaya, Delhi, India, amepewa leseni ya kutoa matibabu nchini Tanzania, na atakuwa akitembelea Dar mara kwa mara kwa ajili kuwaona wagonjwa wake. Tunaleta teknolojia ya kisasa nchini Tanzania ili kukusaidia kupata unafuu. Utaratibu wetu wa kutoa huduma ya uchunguzi na matibabu umeundwa ili kutoa matokeo ya haraka na madhubuti, ya kukurejesha katika maisha yako ya kila siku.

***Teknolojia ya Kisasa, Imefika Nchini Tanzania!***

Mbinu hii ya matibabu ni ya hivi karibuni na imeletwa mahusisi nchini Tanzania na Daktari bingwa wa India.

***Anza kuchukua Hatua sasa ya kuishi bila maumivu***

**Tutumie ujumbe wa WhatsApp kwa +255761460999 au baruapepe amit@hosplan.com ili kuweka miadi yako leo!**

**Hi tech Sai Hospital,
Plot No. 445, mtaa wa Charambe, Upanga, Dar Es Salaam
Tarehe – 22nd , 23rd na 24th Agosti 2024**

# Profesa Janabi aonya ukinzani insulini mwilini

**Na Christina Mwakangale**

UZALISHAJI insulini nyingi mwilini ni chanzo cha ukinzani katika mwili, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi amesema.

Prof. Janabi anafafanua kwamba, insulini huzalishwa na kongosho ambalo hufanya kazi ya kuchukua sukari au wanga uliozidi mwilini na kuvihifadhi vyakula hivyo kama mafuta sehemu mbalimbali kama vile katika ini.

Katika kitabu chake cha 'Mtindo wa Maisha na Afya Yako', bingwa huyo wa matibabu ya moyo anaeleza dalili za ukinzani wa insulini ambazo huchangiwa na ulaji wa chakula usiofaa.

Bingwa huyo ambaye ni Mkaguzi wa Matibabu Usafiri wa Anga aliyeidhinishwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Marekani (FAA-USA), anasema:

"Watu wengi wana ukinzani mwilini lakini hawajui kwa sababu hawajawahi kupima afya zao. Takwimu za kitabibu zinaonesha kuwa watu tisa kati ya 10 wana tatizo la ukinzani wa insulini mwilini.

"Viashiria vya ukinzani wa insulini ni kama vile; kwa wanaume kama upana wa kiuno unazidi inchi 40 na kwa wanawake inchi 35. Hiki ni kielelezo cha ukinzani.

"Shiniko la damu zaidi ya 140/90mmHg ni dalili ya kuwa na ukinzani wa insulini. Ukiwa unatumia dawa za kupunguza shinikizo la juu la damu, hiyo ni dalili pia.

"Wingi wa sukari zaidi ya 100mg/DL nayo ni dalili ya kuwa na tatizo la ukinzani wa insulini mwilini. Matokeo ya kiwango cha insulini ya zaidi ya sita katika kipimo cha maabara ni dalili."

Prof. Janabi anataja wengine wenye dalili za tatizo hilo ni: Kuwa na mafuta mwilini, aina ya 'triglyceride' zaidi ya 150mg na 'high density lipoprotein-HDL' haya ni mafuta salama kwa wanaume chini ya gramu 40 na chini ya gramu 50 kwa wanawake."

Bingwa huyo pia anasema watu wanaotumia dawa za kupunguza kiwango cha lehemu (cholesterol) mwilini na vinyama vilivyoota maeneo tofauti ya mwili kama vile shingoni (skin tags) au madoadoa na mstari mweusi kwenye kwapa (acanthosis nigricans) wana dalili hizo.

"Kwa wanawake kukosa hamu ya tendo la ndoa (reduced libido) na kwa wanaume kukosa nguvu za kiume (erectile dysfunction) pia ni dalili za ukinzani wa insulini.

"Magoti, viungo kuuma au kuwaka moto hali inayomfanya mtu ashindwe kuchuchumaa, kushindwa kufikiria sawasawa, kulala sawasawa (insomnia) na kupanda na kushuka kwa nguvu za mwili (body energy fluctuation) ni dalili zingine," anasema.

Prof. Janabi anasema iwapo watu watapima na kuzitambua dalili za ukinzani wa insulini kabla hazijapevuka, itawasaidia kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza (NCD) kama vile kisukari.

## Mbaroni tuhuma za kutaka kutapeli watawa, kukutwa na pembe za ndovu

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WATU 11 wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Morogoro, wakiwamo wanne wanaodaiwa kukamatwa na vipande 29 vya meno ya tembo katika wilaya za Kilosa na Morogoro na wengine saba wanaotuhumiwa kujaribu kutapeli watawa wa Kanisa Katoliki huko Bigwa, Manispaa ya Morogoro.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, SACP Alex Mkama, alisema hayo mwishoni mwa wkiki wakati akizungumzia operesheni iliyofanywa na polisi kusaka wahalifu katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita.

Alitaja waliokamatwa na vipande vya meno ya tembo kuwa ni Yahaya Bakari (60), mkazi wa Chalinze, mkoani Pwani; Masima Ntumbi, mkazi wa Mlenge, mkazi wa Vianzi, wilayani Mvomero; Juma Zinga (46), mkazi wa Bagamoyo, mkoani Pwani na Mansour Abdallah (40), mkazi wa Dar es Salaam.

Alisema jeshi hilo limewakamata watuhumiwa wengine saba wanaodaiwa kupanga na kushiriki kufanya utapeli katika nyumba ya watawa huko Bigwa Sisters, Manispaa ya Morogoro.

Kamanda Mkama alisema tukio hilo lilitokea Agosti 16 mwaka huu huko Bigwa, watuhumiwa hao wakidaiwa kuingia kwa jinai ndani ya eneo la makazi ya watawa na kunadi madini bandia kwa ajili ya kujipatia fedha.

Alisema watu hao walidanganya kuwa wao walikuwa ni watafiti wa mali kale na kwamba eneo hilo wanaloishi ni sehemu ya utafiti wao.

"Tuliwakamata wakiwa na simu 13, laini za simu 27 za mitandao mbalimbali ya simu zenye usajili wa majina tofauti tofauti ambazo wamekuwa wakizitumia kufanya utapeli," alisema Kamanda huyo.

Aliwataja waliokamatwa kwa tuhuma za utapeli huo kuwa ni Janeth Mhuvile (53), mkazi wa Kigurunyembe, Manispaa ya Morogoro; Samson Amos Can (51), mkazi wa Ruhuwiko, Songea; na Ramadhani Nassor (33), Karimu Mlawa (43), Daniel David (40) Rongido Myovela (66), wote wafanyabiashara na wakazi wa jijini Dar es Salaam pamoja na Joakim Mwinyimvua (65), mkazi wa mkoani Kilimanjaro.

Kamanda huyo alisema mtuhumiwa mwingine, Mussa Nongolo (44) alikamatwa baada ya kudaiwa kudanganya kuwa ni mtumishi wa serikali kwa lengo la kutaka kujipatia kipato kwa watu aliokusudia.

# Mwinyi aona fursa Tamasha la Kizimkazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Tamasha la Kizimkazi ni fursa nyingine kwa Mkoa wa Kusini Unguja kuongeza vivutio vya utalii wa matamasha.

Aliyasema hayo jana wakati akizindua Tamasha la Tisa la Kizimkazi litakalofanyika Agosti 25, mwaka huu, likifunguliwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema katika kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea Zanzibar, serikali imeweka mikakati ya kuongeza vivutio vya utalii kwa kubuni matukio maalum ya kuvutia watalii pamoja na kuimarisha vivutio viliyopo vya asili, yakiwamo mapango, fukwe za bahari na wanyama adimu wanaopatikana Zanzibar pekee.

Alisema Zanzibar imejaaliwa kuwa na urithi wa utamaduni na majengo ya kale kama vile vyumba za ibada za tokea ukoloni, ukiwamo msikiti wa kale wa Kizimkazi.

"Hayo ni miongoni mwa mambo ambayo yanavutia wageni kutoka nchi mbalimbali duniani kuitembelea Zanzibar," alisema.

Rais Dk. Mwinyi alisema serikali ya Mkoa wa Kusini kwa kushirikiana na wananchi pamoja na taasisi mbalimbali, wana wajibu wa kuliendeleza tamasha hilo na kuandaa mipango madhubuti ya kuzidi kuyatangaza matamasha hayo ndani na nje ya nchi sambamba na kubuni fursa zitakazoleta manufaa ya kuwapo matukio hayo.

Alipongeza wananchi wa Wilaya ya Kusini kwa kulipa umuhimu tamasha hilo na kufaidika na fursa mbalimbali za kimaendeleo zinazoambatana na tukio hilo kila mwaka.

Pia aliagiza uongozi wa Mkoa wa Kusini kulitumia tamasha hilo kutangaza na kubainisha fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo.

"Watangazieni wawekezaji fursa zilizopo katika ardhi mlionayo na kuwapo fursa pana ya uwekezaji baharini, ili rasiliamali hizo zilete tija na manufaa kwa wananchi na serikali kwa ujumla," aliagiza.

Alihimiza wawekezaji wa sekta binafsi hasa wamiliki wa hoteli za kitalii kwa kushirikiana na serikali kufanikisha mipango ya maendeleo hasa katika kuimarisha sekta za uchumi, ukiwamo mchango wao wa kuongeza idadi ya watalii nchini, kuchangia Pato la Taifa kwa ulipaji kodi na tozo na utoaji wa ajira kwa vijana wa Zanzibar.

Dk. Mwinyi aliahidi wawekezaji kwamba, serikali itaendelea kuwapa ushirikiano na kuzidi kufungua milango, ili kurahisisha shughuli za uwekezaji nchini hasa katika sekta za utalii, viwanda na biashara.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, alisema viongozi wa nchi wanafanya kazi kubwa ya kuleta maendeleo Bara na Visiwani katika nyanja mbalimbali, kwa kuhakikisha wanaacha alama itakayodumu vizazi na vizazi.

Alisema miradi anayofanya Rais Mwinyi kwa wananchi wa Zanzibar katika sekta ya elimu, afya, miundombinu ya barabara na maji, inayagusa moja kwa moja wananchi na wataendelea kuunga mkono juhudi hizo.

Katibu wa Kamati ya Tamasha hilo, Hindi Juma Ramadhan, alisema licha ya mafanikio ya tamasha hilo, Kijiji cha Kizimkazi kinakabiliwa na changamoto za uhaba wa huduma ya maji safi na salama, umeme mdogo, upungufu wa watoahuduma wa afya, migogoro ya ardhi baina ya wananchi na wawekezaji pamoja na kuporomoko kwa maadili.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiongozana na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila alipowasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam akitoka Cuba, ambako alifanya ziara maalum ya kuboresha uhusiano kati ya nchi hiyo na Tanzania. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Asilimia 85 ya Watanzania wanatumia vitochi - ripoti

**Na Salome Kitomari**

RIPOTI ya Takwimu za Mawasiliano iliyotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), inaonesha matumizi ya simu rununu maarufu vitochi, ni kwa asilimia 85.56 nchini.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, simu za aina hiyo zinazotumika ni 52,825,801 zikifuatwa na simu janja (smart phones) 20,118,846.

Licha ya idadi ya matumizi ya simu hizo kuwa kubwa, idadi ya watu wanaozitumia imepungua kutoka asilimia 85.62 mwishoni mwa Desemba 2023 hadi asilimia 85.56 Machi 2024.

Ripoti hiyo ya robo ya tatu ya mwaka 2013/24, inaonesha idadi ya laini za Intaneti imeongezeka kutoka milioni 35.9 kwa robo mwaka iliyoishia Desemba 2023 hadi milioni 36.8 kwa robo mwaka iliyoishia Machi 2024.

Ripoti hiyo inabainisha kuwa kufikia Machi 2024, idadi ya watu wanaotumia simu janja imeongezeka hadi asilimia 32.59 kutoka 32.13 iliyorekodiwa mwishoni mwa Desemba 2023.

Kwenye takwimu za usajili wa fedha mtandao, idadi ya akaunti za fedha mtandao ambazo zimetumika angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita iongezeka kutoka akaunti milioni 52.9 katika robo mwaka iliyoishia Desemba 2023 hadi milioni 53 Machi 2024.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, miamala ya fedha mtandaoni kwa miaka mitano iliyopita (2019-2023), imeongezeka kutoka Sh. bilioni tatu mwaka 2019 hadi bilioni 5.3, sawa na asilimia 19 ya ukuaji kwa kila mwaka, na kwamba wastani wa miamala kwa kila mteja umepungua kutoka miamala 117 mwaka 2019 hadi 100 mwaka 2023.

Ripoti hiyo imebainisha Intaneti ya simu ndiyo njia maarufu zaidi ya kupata Intaneti, ikiwa na laini 24,431,561 huku teknolojia ya 2G ikiwa na matumizi makubwa, ikiwa na laini 12,256,233, teknolojia za faiba nyumbani na faiba ofisini zina idadi ndogo ya laini ambazo ni 49,163 na 5,126, mtawalia.

Aidha, wigo wa 3G, 4G na 5G umepanuka kufikia asilimia 88, 80 na 13 ya watu nchini, huku eneo lillilofikiwa na intaneti ya kasi 3G, 4G na 5G ni asilimia 72, 64 na moja, mtawalia.

"Wastani wa ongezeko la kila mwaka la asilimia 9.8 la idadi ya laini zinazotumia huduma ya Intaneti kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Laini zinazotumia Intaneti ziliongezeka kutoka milioni 25.8 mwaka 2019 hadi milioni 35.9 mwaka 2023," inaeleza sehemu ya ripoti hiyo.

Kuhusu matukio ya ulaghai, ripoti hiyo inaonesha kuwa majaribio ya ulaghai yamepungua kwa watoahuduma wote kwa angalau asilimia 15 isipokuwa Vodacom ambaye yameongezeka kwa asilimia 30 kutoka majaribio 2,876 katika robo mwaka inayoishia Desemba hadi majaribio 3,735 katika robo inayoishia Machi 2024.

Vilevile, majaribio ya ulaghai kimkoa, mikoa ya Rukwa na Morogoro inayoongoza, ikiwa na zaidi ya theluthi moja ya majaribio yote ya ulaghai nchini huku Mbeya, Dar es Salaam na Tabora zinafuata kwa majaribio ya ulaghai kwa zaidi ya asilimia moja hadi 10.

Mikoa ya Kaskazini Pemba, Kusini Unguja na Kusini Pemba ina idadi ndogo ya majaribio, kila mkoa ulirekodi asilimia 0.01.

# Taarifa ya Mkutano Mkuu

Pamoja tunaweza

## Vodacom Tanzania Public Limited Company

(Imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
(Namba ya usajili 38501)
(ISIN: TZ1996102715 Ticker code: VODA)
('Vodacom Tanzania' au 'Kampuni')

Taarifa inatolewa kuwa, mkutano mkuu wa nane wa Kampuni kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2024 utafanyika kwa njia ya kielektroniki siku ya Jumatano tarehe 11 Septemba 2024 kuanzia saa nne asubuhi. Mkutano huu utajadili yafuatayo:

### 1. Kuthibitisha kumbukumbu

Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano mkuu wa saba uliofanyika tarehe 22 Septemba 2023.

#### Azimio la kawaida namba 1

"ILIAMULIWA KUWA kumbukumbu za mkutano mkuu wa saba uliofanyika tarehe 22 Septemba 2023 zimethibitishwa."

Nakala za kumbukumbu zinapatikana kwenye tovuti ya Kampuni **www.vodacom.co.tz/annual-general-meeting**.

### 2. Kupitisha taarifa za fedha za mwaka zilizokaguliwa

Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2024.

#### Azimio la kawaida namba 2

"ILIAMULIWA KUWA taarifa za fedha zilizokaguliwa za Kampuni, pamoja na taarifa ya wakaguzi huru na ya wakurugenzi kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2024, zimepokelewa na kupitishwa."

Nakala za taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Machi 2024 zinapatikana katika tovuti ya Kampuni **www.vodacom.co.tz/financials**.

### 3. Uchaguzi wa wakurugenzi

Kwa kupitia maazimio tofauti:

3.1 Bw Dejan Kastelic aliteuliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji kwa mujibu wa ibara ya 86 ya Katiba ya Kampuni, kujaza nafasi iliyojitokeza katika Bodi na kuendelea kutekeleza majukumu ya kiofisi hadi mkutano wa kawaida unaofuata, na hivyo anastahili kuchaguliwa.

3.2 Bw Haytham Ammar aliteuliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji kwa mujibu wa ibara ya 86 ya Katiba ya Kampuni, kujaza nafasi iliyojitokeza katika Bodi na kuendelea kutekeleza majukumu ya kiofisi hadi mkutano wa kawaida unaofuata, na hivyo anastahili kuchaguliwa.

3.3 Bw Matimba Mbungela, Bw Diego Gutierrez and Bi Raisibe Morathi wanapaswa kustaafu katika mkutano huu kwa mujibu wa ibara 104 na 105 za Katiba ya Kampuni. Ibara hizo zinabainisha kuwa licha ya kustaafu, wanaweza kuchaguliwa kwa mara nyingine tena kuwa wakurugenzi.

#### Azimio la kawaida namba 3

"ILIAMULIWA KUWA Bw Dejan Kastelic amechaguliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji."

#### Azimio la kawaida namba 4

"ILIAMULIWA KUWA Bw Haytham Ammar amechaguliwa kuwa mkurugenzi asiye mtendaji."

#### Azimio la kawaida namba 5

"ILIAMULIWA KUWA Bw Matimba Mbungela amechaguliwa tena kuwa mkurugenzi asiye mtendaji."

#### Azimio la kawaida namba 6

"ILIAMULIWA KUWA Bw Diego Gutierrez amechaguliwa tena kuwa mkurugenzi asiye mtendaji."

#### Azimio la kawaida namba 7

"ILIAMULIWA KUWA Bi Raisibe Morathi amechaguliwa tena kuwa mkurugenzi asiye mtendaji."

### 4. Uteuzi wa Ernst & Young kuwa wakaguzi huru wa Kampuni

Kuteua kampuni ya Ernst & Young Inc., kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji, kuwa wakaguzi huru wa Kampuni na kushikilia nafasi hiyo hadi mwisho wa mkutano mkuu ujao wa mwaka.

#### Azimio la kawaida namba 8

"ILIAMULIWA KUWA Ernst & Young Inc. imeteuliwa kuwa mkaguzi huru wa Kampuni na kushikilia nafasi hiyo hadi mwisho wa mkutano mkuu ujao wa mwaka."

### 5. Uteuzi wa wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji

Kupitia maazimio tofauti na kwa mujibu wa kifungu cha 32(f) cha Katiba ya Kampuni, Bi Margaret Ikongo, Bi Thembeka Semane na Bi Kanini Mutooni wakiwa wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji wachaguliwe kuendelea kuwa wajumbe.

#### Azimio la kawaida namba 9

"ILIAMULIWA KUWA Bi Margaret Ikongo amechaguliwa kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji."

#### Azimio la kawaida namba 10

"ILIAMULIWA KUWA Bi Thembeka Semane amechaguliwa kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji."

#### Azimio la kawaida namba 11

"ILIAMULIWA KUWA Bi Kanini Mutooni amechaguliwa kuendelea kuwa mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji."

### 6. Gawio

Kuidhinisha gawio la mwisho la Shi 11.93 kwa kila hisa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2024 kama ilivyopendekezwa na wakurugenzi. Gawio litalipwa kabla au Jumatano ya tarehe 16 Oktoba 2024 kwa wanahisa waliosajiliwa kwenye kitabu cha usajili baada ya kufunga biashara ya hisa tarehe 15 Agosti 2024.

#### Azimio la kawaida namba 12

"ILIAMULIWA KUWA gawio la Shi 11.93 kwa hisa ya kawaida kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Machi 2024 limeidhinishwa."

### 7. Ada ya wakurugenzi

Kuidhinisha ada ya wakurugenzi wasio watendaji ya dola za Kimarekani 477 000 hadi hitimisho la mkutano mkuu ujao wa mwaka, ili kuiwezesha Kampuni kuwavutia watu wenye uwezo, ujuzi na uzoefu unaotakiwa ili kutoa mchango unaofaa kwa Kampuni. Hakuna mapendekezo ya mabadiliko ya ada.

#### Azimio la kawaida namba 13

"ILIAMULIWA KUWA kiwango cha ada ya mwaka ya wakurugenzi wasio watendaji cha dola za Kimarekani 477 000 kimeidhinishwa kwa mchanganuo ufuatao:

| | Pendekezo la ada Dola ya Marekani[1] | Ada ya sasa Dola ya Marekani |
|---|---|---|
| Mwenyekiti wa Bodi | **150 000** | 150 000 |
| Mjumbe wa Bodi | **30 000** | 30 000 |
| Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | **15 000** | 15 000 |
| Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji | **8 000** | 8 000 |
| Mwenyekiti wa Kamati ya Ujira | **12 000** | 12 000 |
| Mjumbe wa Kamati ya Ujira | **4 000** | 4 000 |
| Mjumbe wa Kamati ya Uteuzi | **3 000** | 3 000 |

1. Ada hii inajumuisha kodi zote ikijumuisha kodi ya zuio, inayolipwa kwa shilingi ya Kitanzania kwa wakurugenzi wazawa, randi ya Afrika Kusini kwa wakurugenzi wa Afrika Kusini na dola ya Marekani kwa wakurugenzi wengine. Ada hii inalipwa kila robo mwaka.

## Wasifu wa Wajumbe wa Bodi

**Dejan Kastelic (43)**

Mkurugenzi asiye mtendaji

*Shahada ya Sayansi katika Uhandisi Umeme kutoka Chuo kikuu cha Maribo kilichopo Slovenia; Alisoma Chuo Kikuu cha Harvard kilichoko Boston Marekani na INSEAD*

Bw Kastelic aliteuliwa kuwa Afisa Mkuu wa Teknolojia wa Vodacom Group, Afrika Kusini mwezi Agosti 2020. Kabla ya kujiunga na Vodacom, alikuwa Afisa Mkuu wa Teknolojia na Habari katika kampuni ya PT Indosat Ooredoo TBK, sehemu ya kampuni ya Kundi la makampuni ya Ooredoo huko Qatar. Aidha, aliwahi kuwa Mkurugenzi wa kampuni ya Indosat, Singapore na ni Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi wa Posta Slovenije d.o.o. Bw Kastelic alianza kazi katika kampuni ya simu Amis Ltd hadi kufikia nafasi ya Afisa Mkuu wa Technolojia. Mwaka 2009 alihamia kampuni ya IBM Ulaya Mashariki na Kati kama Meneja Usimamizi wa Rasilimali. Mwaka 2012 alijiunga na kampuni ya Telkom Austria akiwa kama Mkurugenzi Mtendaji na Afisa Mkuu wa Teknolojia na Habari na baadaye akawa Mkurugenzi wa Kundi na Afisa Mkuu wa Technolojia na Habari akisimamia kampuni za simu – Vip mobile, Serbia na Si.Mobil Slovenia. Mwaka 2015, alihamishiwa kampuni ya Mobiltel Bulgaria hadi alipoteuliwa kwenye nafasi aliyoishikilia mwanzo katika kampuni ya Indosat. Bw Kastelic pia ni mkurugenzi wa bodi ya Vodacom Msumbiji na Vodacom Lesotho.

**Haytham Ammar (42)**

Mkurugenzi asiye mtendaji

*Shahada ya Uhasibu na Usimamizi wa Biashara, Cheti cha Taaluma ya Uhasibu*

Haytham aliteuliwa kuwa Afisa Mkuu wa Fedha wa Makampuni Tanzu ya Vodacom mwezi Juni 2024. Kabla ya kujiunga na Vodacom, alikuwa Afisa Mkuu wa Fedha wa M-Pesa Africa. Aidha, aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Fedha wa Vodafone Ghana ambapo alitoa mchango mkubwa katika kufanya mageuzi ya kibiashara yaliyopelekea ukuaji kiuendeshaji na kifedha huku akichochea ongezeko la thamani ya biashara kulingana na rasilimali chache zilizokuwepo. Anasifiwa pia kwa kuboresha mazingira ya udhibiti wa mapato, ugavi, usimamizi wa madeni, na uwasilishaji wa taarifa za kifedha. Haytham alianza kufanya kazi na Vodafone mwaka wa 2007 alipojiunga na Vodafone Misri, ambapo majukumu yake yalihusisha nyanja mbalimbali ikiwemo Mipango ya Fedha, Uwasilishaji wa Taarifa za Kifedha, na Mipango Maamuzi, akiisaidia timu ya Misri katika kupanga na kutekeleza mipango mikakati muhimu kama vile ujenzi wa minara ya teknolojia ya 4G, maboresho ya kidigitali, na kuchochea ufanisi katika gharama za matumizi.

**Raisibe Morathi (55)**

Mkurugenzi asiye mtendaji

*Shahada ya Uzamili ya Filosofia, Stashahada ya juu ya masuala ya kodi kutoka Chuo Kikuu cha Wits, Mhitimu wa programu ya menejimenti ya INSEAD (Ufaransa), Cheti cha Taaluma ya Uhasibu ya Afrika Kusini (CA, SA)*

Raisibe aliteuliwa kuwa Afisa Mkuu wa Fedha wa Vodacom Group Limited mwezi Novemba 2020. Alijiunga na Vodacom akitokea Nedbank Group ambapo alikuwa Afisa Mkuu wa Fedha tangu Septemba 2009. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka 27 katika huduma za fedha katika mashirika mbalimbali makubwa huko Afrika Kusini, ikiwa ni pamoja na Nedbank Group, Sanlam Group na Industrial Development Corporation. Raisibe pia ni mkurugenzi asiye mtendaji wa bodi za Vodacom Afrika Kusini na Safaricom PLC.

**Diego Gutierrez (48)**

Mkurugenzi asiye mtendaji

*Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara na Masoko, Chuo Kikuu cha Católica, Bolivia*

Diego aliteuliwa kuwa Afisa Mkuu wa Uendeshaji wa Vodacom International Business mwezi Agosti 2017. Diego ana uzoefu wa zaidi ya miaka 20 katika shughuli za kimataifa katika sekta ya mawasiliano ya simu hususan kwenye masoko yanayoibukia huko Latini Amerika, Afrika na visiwa vya Karibi. Ana uzoefu uliothibitika wa kufanya mageuzi ya kibiashara na kuwezesha ongezeko la ufanisi wa uendeshaji, kupitisha makampuni katika vipindi vigumu vya mabadiliko na kutafsiri mikakati ya mashirika kuwa matokeo ya uendeshaji yanayoonekana. Bw Gutierrez pia ni mkurugenzi wa bodi ya Vodacom Congo DRC, Vodacom Lesotho, Vodacom Msumbiji, M-Pesa Africa na M-Pesa Africa Kusini.

**Matimba Mbungela (52)**

Mkurugenzi asiye mtendaji

*Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Kwazulu Natal, Shahada ya Utawala, Chuo Kikuu cha Venda, Stashahada ya Juu ya Rasilimaliwatu, Chuo Kikuu cha Cape Town, Mhitimu wa Programu ya Vodafone kwenye ubora wa masuala ya rasilimaliwatu*

Matimba aliteuliwa kuwa Afisa Mkuu wa Rasilimali Watu wa Vodacom Group Limited mwezi April 2014. Kabla ya kushika nafasi hii, alikuwa Afisa Mkuu wa Rasilimali Watu wa Vodacom South Africa hadi Aprili 2014. Matimba amefanya kazi ndani ya Vodacom/Vodafone Group tangu 2003 akishikilia nafasi mbalimbali katika Kitengo cha Rasilimaliwatu. Kwa miaka mitatu alifanya kazi Vodafone kama Mkuu wa Kanda ya Afrika, Mashariki ya Kati na Asia Pasifiki "AMAP" akihusika na Ufanisi na Mabadiliko na pia kama Mkuu wa Vipaji wa Kanda. Kabla ya hapo alikuwa anashughulikia Usimamizi wa Vipaji katika Vodacom kwa miaka sita ambapo alitekeleza kwa mafanikio kujumuishwa kwa mkakati wa vipaji katika mkakati wa dunia wa Vodafone. Uzoefu wake wa siku za nyuma ni pamoja na kufanya kazi za Afisa Rasilimaliwatu katika kampuni za BMW Afrika Kusini na Unilever. Matimba anawakilisha Vodacom Employee Trust ('Siyanda') katika Bodi ya YeboYethu, pia ni Mkurugenzi Asiye Mtendaji wa Vodacom Msumbiji na Vodacom Lesotho na ni mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Unisa GSBL.

**Margaret Ikongo (66)**

Mkurugenzi huru

Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii

*Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu Huria, Tanzania. Cheti cha Kimataifa cha Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Taasisi ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Uingereza. Diploma ya Kimataifa ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi na Mjumbe Mhitimu wa Taasisi ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi, Uingereza. Mwanachama katika Taasisi ya masuala ya Bima, Uingereza*

Margaret aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Pia ni mjumbe wa bodi ya wakurugenzi ya Actuarial and Risk Consulting na Metrolife and Meticulus Insurance. Kabla ya hapo, Margaret alikaa kwenye Bodi ya benki ya NMB na AAR Insurance Tanzania, pamoja na Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). Margaret ana uzoefu mkubwa katika masuala ya fedha na utawala bora akiwa ameupata kutokana na kufanya kazi katika sekta ya bima ambapo alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima la Taifa kwa kupindi cha miaka kumi. Margaret pia alikuwa mshauri wa Kamishna wa Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania pamoja na Kaimu Mkuu wa Kurugenzi ya Ufundi.

**Thembeka Semane (48)**

Mkurugenzi huru

Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii

*Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Monash; Stashahada ya Juu katika Usimamizi wa Biashara, Chuo Kikuu cha Biashara cha Pretoria Gordon; Shahada ya Biashara katika Uhasibu; Chuo Kikuu cha Transkei (Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Walter Sisulu kwa sasa); Mwanachama wa Taasisi ya Taaluma ya Benki ya Afrika Kusini*

Thembeka aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Novemba 2017. Thembeka ana uzoefu katika masuala ya biashara ukihusisha mikakati ya mashirika, utekelezaji wa mifumo ya biashara, miradi yenye thamani kubwa, utekelezaji na ufuatiliaji, utawala bora na vilevile usimamizi wa fedha. Thembeka ni mkurugenzi wa Linea Consulting (Pty) Ltd, mjumbe wa Kamati ya Udhibiti ya ACASA & ATNS, akiripoti kwa Waziri wa Usafirishaji wa Afrika Kusini na pia, ni mjumbe wa Baraza la ICASA. Thembeka anafanya kazi kama mjumbe wa bodi wa Idara ya Makazi EAAB, ambapo ni Mwenyekiti wa Kamati yake ya Fedha na Uwekezaji na pia, ni mjumbe wa Kamati za Ukaguzi na Dharura pamoja na ya Rasilimali watu na Ujira. Pia, Thembeka ni mjumbe wa bodi na mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Dharura na Kamati ya Ujira ya Mamlaka ya usimamizi wa Mbuga za Wanyama za Afrika Kusini. Vilevile, Thembeka ni mjumbe wa South African Heritage Resource Agency na Kamati ya Uthibiti na Usimamizi wa Utendaji wa Manispaa ya Sol Platje.

**Kanini Mutooni (48)**

Mkurugenzi huru

Mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Dharura na Utekelezaji na anatambuliwa kuwa mtaalamu wa fedha kwa madhumuni ya kamati hii

*Elimu ya utekelezaji wa Sera za Kimataifa, Shule ya masuala ya kiserikali ya Harvard. Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara, Shule ya Biashara Cass ya Chuo Kikuu cha Jiji la London. Diploma ya masuala ya Dhamana (Uingereza). Cheti cha Taaluma ya Usimamizi katika Uwekezaji (Uingereza). Cheti cha Taaluma ya Uhasibu (ACCA), Uingereza. Shahada ya Biashara, Chuo Kikuu cha Kikatoliki, Kenya*

Kanini aliteuliwa kuwa mkurugenzi huru wa Vodacom Tanzania mwezi Oktoba 2022. Kanini ni Mkurugenzi Mtendaji wa Draper Richards Kaplan Foundation kwa Afrika. Hivi sasa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Draper Richards Kaplan Foundation akisimamia Afrika. Pia ni mjumbe katika Bodi za Financial Sector Deepening Africa (FSDA); MCE Social Capital, the United Nations Capital Development Fund, Africa Enterprise Challenge Fund, Amref Health Innovation na CDC UK PLC. Kabla ya hapo, Kanini alikuwa mjumbe wa Bodi katika benki za uwekezaji huko Uingereza na Marekani ikiwa ni pamoja na Bank of America-Merrill Lynch na Dresdner Kleinwort Benson.

---

## Tarehe ya kufunga rejesta

Tarehe ya kufungwa rejesta ya wanahisa wa Kampuni kwa madhumuni ya kustahili kuhudhuria, kushiriki na kupiga kura kwenye mkutano mkuu wa mwaka ni Jumatano 4 Septemba 2024.

## Ushiriki kwa njia ya kielektroniki

Mkutano mkuu wa mwaka utafanyika kwa njia ya kielektroniki kama ilivyoainishwa kwenye kifungu 29 na 63 cha Katiba ya Kampuni. Wanahisa waliosajiliwa kwenye rejesta hadi kufikia tarehe ya kufunga rejesta hiyo, watapokea ujumbe mfupi wa maneno wenye taarifa za kuwawezesha kuingia kwenye mkutano huo. Mkutano mkuu wa mwaka utaoneshwa mubashara kupitia kiunga cha wavuti kwenye vifaa janja vilivyounganishwa na intaneti. Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya Kampuni **www.vodacom.co.tz/annual-general-meeting**.

Wanahisa watawajibika kwa gharama za data na mtandao. Kampuni haitawajibika na upotevu wa mawasiliano kutokana na matatizo ya kimtandao/kuishiwa muda wa hewani/kukatika kwa umeme/na matatizo ya kiufundi ya kielektroniki yanayoweza kuathiri ushiriki wa mwanahisa kwenye mkutano mkuu mwaka kwa njia ya mtandao.

Wanahisa wanahimizwa kutuma maswali yatokanayo na maazimio yaliyopo kwenye taarifa hii kabla ya mkutano mkuu kwenda kwenye barua pepe **investorrelations@vodacom.co.tz** kabla ya Ijumaa ya tarehe 6 Septemba 2024 saa 4:00 asubuhi. Majibu ya maswali hayo yatatolewa katika mkutano mkuu. Uwasilishaji wa maswali haumzuii mwanahisa kuuliza maswali siku ya mkutano mkuu.

## Mahudhurio

Wanaostahili kuhudhuria, kuzungumza na kupiga kura kwenye mkutano mkuu wa mwaka ni wanahisa tu.

Wanahisa wanaweza kuteua wawakilishi kuhudhuria, kutoa maoni na kupiga kura kwa niaba yao. Mwakilishi si lazima awe mwanahisa wa Kampuni. Fomu ya uwakilishi iliyojazwa, inayopatikana kwenye tovuti ya Kampuni, pamoja na risiti ya uwekezaji ya DSE ya mwanahisa, kitambulisho cha taifa/kura/leseni ya udereva na taarifa za mawasiliano vitumwe kwa barua pepe kwenda **investorrelations@vodacom.co.tz** au viwasilishwe kwa Katibu wa Kampuni, ghorofa ya 15, Vodacom Tower, Ursino Estate, Kiwanja namba 23, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam, Tanzania kabla ya saa 4:00 asubuhi Ijumaa ya tarehe 6 Septemba 2024. Kujazwa kwa fomu ya mwakilishi hakumzuii mwanahisa yeyote kuhudhuria mkutano mkuu wa mwaka.

Upigaji kura utaendeshwa kulingana na Katiba na kanuni za Kampuni. Maazimio ya kawaida yatakayopitishwa katika mkutano mkuu huu yatapaswa kuungwa mkono na zaidi ya 50% ya kura za wanahisa. Azimio maalum litapaswa kuungwa mkono na angalau 75% ya kura za wanahisa.

Wanahisa wenye hisa zisizo kwa majina yao lazima wawapatie watunzaji au wawakilishi wao maelekezo ya kupiga kura katika mkutano mkuu wa mwaka. Kama mtunzaji au mwakilishi wako hatapokea maelekezo kutoka kwako, kama itakavyokuwa, itabidi kufanya maamuzi kulingana na mamlaka uliyoyatoa kwake.

Wanahisa wanahimizwa kuendelea kufuatilia tovuti ya Kampuni ili kupata taarifa zaidi zinazohusiana na mkutano mkuu wa mwaka.

Imeidhinishwa na Bodi.

**Caroline M Mduma**
Katibu wa Kampuni
19 Agosti 2024

STUDIO5

HABARI KITAIFA

## Vigogo wakuna vichwa mmomonyoko wa maadili

**Na Julieth Mkireri,**
MKURANGA

KUPOROMOKA kwa maadili nchini kumechangiwa na kupungua elimu ya imani, hivyo jamii kutokuwa na hofu ya Mungu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Mohamed Mwera aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kikao cha Baraza la Madiwani.

Mwera alisema jamii inatakiwa kubadilika na kusimamia watoto wao kiimani, akiamini kufanya hivyo kutasaidia jamii kuwa na hofu ya Mungu na watoto kusimama kwenye maadili.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Mkuranga, Omari Mwanga, akiwa katika kikao hicho cha Baraza la Madiwani aliomba madiwani kushirikiana na viongozi wengine kuhakikisha katika mikutano yao ajenda ya maadili ipewe kipaumbele.

"Tunatamani watoto wetu wa sasa miaka ijayo wawe miongoni mwa viongozi lakini wakishafanyiwa vitendo vya ubakaji wakiwa wadogo, inasababishia kupoteza mwelekeo na ndoto zao za baadaye.

"Suala hili kila mtu anatakiwa kulichukua kwa uzito wake kuondoa mmomonyoko wa maadili unaoendelea katika jamii zetu," alisema.

Akizungumzia utekelezaji miradi ya maendeleo, Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Hadija Nasri, aliwataka viongozi kuwa na matumizi mazuri ya fedha za mapato ya ndani kwa kutekeleza miradi inayotatua kero za wananchi.

"Sisi tuna mapato makubwa ya ndani, fedha zinatakiwa kutumika kujenga miradi mikubwa inayoonekana kama ilivyo kwenye fedha zinazotoka Serikali Kuu, tuzingatie kusimamia vizuri fedha za mapato ya ndani ili hata tukiulizwa tunacho cha kukionesha," alisema.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Waziri Kombo, alisema katika kutekeleza bajeti wanayoipitisha, wanasimamia fedha zake kama zilivyopangwa na kwamba katika mwaka wa fedha 2023/24 mapato yalikusanywa kwa asilimia 102.

Kombo alitaja miradi mikubwa iliyotekelezwa, ikijumuisha zahanati mpya sita zilizojengwa kutokana na mapato ya ndani na wanaendelea kubainisha maeneo yenye vikwazo na kupeleka miradi ya maendeleo.




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (katikati), akiongozana na viongozi wengine wa serikali na Benki ya CRDB kuanza mbio za kilometa tano katika kilele cha msimu wa tano wa CRDB Bank Marathon zilizofanyika viwanja vya Farasi 'The Green Grounds' jijini Dar es Salaam jana na kuhudhuriwa na washiriki zaidi ya 8,000. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Biteko apongeza marathon ya CRDB kusaidia watoto, kinamama na vijana

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, amepongeza Taasisi ya CRDB Bank Foundation kwa kuendelea kuandaa mbio za marathon ambazo mapatio yake yameelekezwa kusaidia jitihada za serikali kuboresha sekta ya afya, kusaidia wenye uhitaji na kukuza ustawi wa jamii.

Dk. Biteko alitoa pongezi hizo jana wakati wa kilele cha msimu wa tano wa CRDB Bank Marathon ambapo Sh. milioni 350 zimekusanywa kwa ajili ya kusaidia watoto wenye uhitaji wa upasuaji wa moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), huduma za afya kwa kinamama wenye ujauzito hatarishi katika Hospitali ya CCBRT na uwezeshaji vijana.

"Niwapongeze kwa kuendelea kusaidia matibabu ya kinamama na watoto wetu. Kinamama ndio wamebeba uchumi wa taifa letu. Lakini pia kinamama ndio waangalizi wa familia zetu hususani watoto. Hivyo, ukiimarisha afya ya mama na watoto umeimarisha afya ya taifa," alisema Dk. Biteko.

Naibu Waziri Mkuu, Biteko alisema serikali na Watanzania wanaona jitihada hizo zinazofanywa na Benki ya CRDB kupitia CRDB Bank Foundation.

Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, alisema CRDB Bank Marathon imesaidia kwa kiasi kikubwa kuchochea ari ya michezo nchini.

Dk. Ndumbaro alisema mbio hizo zimekuwa jukwaa muhimu kwa wanariadha nchini kuonesha vipaji vyao katika jukwaa la kimataifa kwa kuwa mbio hizo zimesajiliwa kimataifa na Shirikisho la Upimaji Mbio Kimataifa (AIMS) na Shirikisho la Riadha Duniani (World Athletic).

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema kati ya fedha zilizokusanywa, Sh. milioni 100 zitakwenda kusaidia watoto wenye uhitaji wa upasuaji JKCI, Sh. milioni 100 zitasaidia huduma za afya kwa kinamama wenye ujauzito hatarishi Hospitali ya CCBRT na Sh. milioni 150 zitaelekezwa kwenye uwezeshaji vijana.

Katika mbio hizo, zawadi za jumla ya Sh. milioni 98.7 zimetolewa kwa washindi 60 wa mbio za kilometa 42, 21, 10 na tano pamoja na mbio za baiskeli za kilometa 65.

Mwenyekiti wa Bodi ya CRDB Bank Foundation, Martin Warioba, alisema jumla ya washiriki waliojiandikisha mwaka huu ni 8,000 huku akisema lengo la mwaka kesho ni kupata washiriki 10,000 Tanzania, huku malengo ya washiriki Burundi na DRC wakiwa ni 3,000 kwa kila nchi.

> **"Niwapongeze kwa kuendelea kusaidia matibabu ya kinamama na watoto wetu. Kinamama ndio wamebeba uchumi wa taifa letu. Lakini pia kinamama ndio waangalizi wa familia zetu hususani watoto. Hivyo, ukiimarisha afya ya mama na watoto umeimarisha afya ya taifa," alisema Dk. Biteko.**

Mbio hizo zilizofanyika Dar es Salaam jana ni za tatu baada ya zile zilizofanyika DRC na Burundi. DRC mbio hizo zilifanyika Agosti 4, mwaka huu ambako Dola za Marekani 50,000 zilikusanywa kusaidia kuboresha huduma za afya kwa watoto katika Hospitali ya Jason Sendwe jijini Lubumbashi.

Kwa upande wa Burundi, mbio hizo zilifanyika Agosti 11, mwaka huu ambako Faranga za Burundi milioni 120 zilikusanywa kusaidia waathirika wa mafuriko Mkoa wa Gatumba.

Akizungumza wakati wa kutangaza matokeo ya mbio hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Esther Mwambapa, alipongeza washindi wa mbio hizo na kushukuru washirika wa mbio hizo, wakiwamo kampuni za bima Sanlam na Alliance Life ambao ni washirika wakuu wa mbio hizo.

"Tunawashukuru sana washirika wetu na wakimbiaji wote kwa kuungana nasi katika juhudi za kusambaza tabasamu kwa watoto walioathirika," alisema Tully.

Washindi wa mbio hizo, Km 42 upande wa wanawake ni Joylyce Kemuma kutoka Kenya, upande wa wanaume mshindi ni Moses Nengichi kutoka Kenya. Kilometa 21 upande wa wanawake ni Sara Makera kutoka Tanzania, na upande wa wanaume ni Joseph Panga kutoka Tanzania.

Km 10 upande wa wanawake, mshindi ni Hamida Nasor kutoka Tanzania na upande wa wanaume ni Mao Hindo Ako kutoka Tanzania.

Sara Makera, mshindi wa mbio za Km 21 upande wa wanawake, alieleza furaha yake kushiriki katika mbio hizo na kusema kuwa ushindi wake ni sehemu ya kusaida matibabu ya watoto wenye matatizo ya moyo na matibabu ya kinamama wenye ujauzito hatarishini hospitalini CCBRT.

"Mimi kama mwanamke, ninajisikia faraja kubwa kushiriki kusambaza tabasamu kwa watoto na kinamama. Watu wanapaswa kufahamu kuwa afya bora ni haki ya kila mtoto na kinamama pia hawastahili kupoteza maisha wakati wa kujifungua. Tunawashukuru CRDB Bank Foundation kwa kutuunganisha pamoja katika juhudi hizi," alisema.

# Nipashe
MWANGA WA JAMII

## TFF isipuuzie kilio cha wadau, mdhamini mmoja timu saba

**HATA** kama yatapuuzwa au wahusika kuziba masikio, lakini kuna kelele na manung'uniko kutoka kwa mashabiki na wadau wa soka kwenye mitandao ya kijamii na kupitia baadhi ya vyombo vya habari, kuhusu Kampuni ya GSM kudhamini zaidi ya timu moja kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wala huwezi kuuliza kuwa yanatoka wapi zaidi ya wanachama na mashabiki wa Simba, ambao wanaona hakuna haki kwa kampuni hiyo kudhamini timu takriban sita hivi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hapa hatusemi wapo sahihi au la, lakini manung'uniko yanapozidi siku hadi siku, yanapaswa wenye mamlaka na soka la Tanzania Bara kukaa chini na kutafakari kwa kina, kwani walalamikaji wanaonekana kuwa na hoja.

Tumewasikia baadhi ya viongozi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF) na Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB) kwa nyakati tofauti wakisema hakuna kanuni inayozuia na pia udhamini huo unaziingizia timu ambazo nyingi hazina uwezo mkubwa wa kipato.

Kwa hilo la kipato tunadhani wapo sahihi, lakini ni lazima liangaliwe kama hicho kipato kipo katika njia sahihi ambayo haiwezi kwa namna yoyote kuhusika katika upangaji wa matokeo.

Hebu hapa twende sawa, klabu ya Arsenal inadhaniwa na Shirika la Ndege la Emirates na ni klabu pekee nchini humo inayodhaminiwa na shirika hilo, zingine nje ya hapo ni PSG ya Ufaransa, AC Milan ya Italia na Real Madrid ya Hispania.

Hata hivyo, japo timu hizo zinaweza kukutana kwenye michuano ya Ulaya, lakini udhamini wa Emirates hauna chembe yoyote ya vinasaba na moja kati ya klabu hizo mbali na udhamini kibiashara, hivyo hautiliwi shaka kwamba kunaweza kuwapo na aina yoyote ya upangaji wa matokeo kwani haijawekeza kwenye klabu yoyote zaidi ya kudhamini tu.

Ukiangalia hapa nchini GSM, inaonekana amejikita kabisa katika Klabu ya Yanga. Ndiyo inayohusishwa na sapoti kubwa katika usajili na kuiendesha timu, huku ikionekana kusaidia pakubwa mchakato wa uwekezaji.

Hivyo, inakuwaje kampuni hiyo hiyo inakwenda kudhamini timu zingine kwenye Ligi Kuu? Hata kama hakuna kanuni, hata busara tu haielekezi? Hivi mtu kama Mohamed 'Mo' Dewji akianza kudhamini timu za Ligi Kuu, wakati tayari anautaka uwekezaji Klabu ya Simba, unatarajia nini baada ya kuzidhamini zingine?

Kama ambavyo walioainisha kwamba kunaweza kuwapo na upangaji wa matokeo kwa kampuni tu ambayo haipo kwenye klabu yoyote kudhamini zaidi ya timu moja kwenye ligi moja, inakuajie kwa Ligi Kuu Bara?

Kwa mtazamo wetu tunaona kama tunaanza kurudi nyuma, wakati tulishatoka huko zamani. Tunakumbuka kulikuwa na timu za Mgambo JKT, JKT Ruvu, Ruvu Shooting, zote zikimilikiwa na taasisi moja ya Jeshi la Kujenga Taifa na zilikuwa Ligi Kuu, lakini moja kati ya maazimio ya Bagamoyo mwanzoni mwa miaka ya 2000 kutoka FIFA, ulizitaka klabu zote za aina hiyo kuwa na timu moja tu kwenye ligi.

FIFA iliona hakutakuwa na haki na usawa, kwani JKT Ruvu kama inahitaji pointi moja ili isishuke daraja na inacheza na Ruvu Shooting ambayo ipo salama kwa alama zake, haiwezi kuikosa kwa sababu mwajiri wao ni mmoja, hivyo kuzuia haki kwa timu ambazo hazina timu zenye vinasaba na nyingine kushinda kwa haki.


Ndiyo maana kwa sasa kuna JKT Tanzania, pia kuna Polisi Tanzania, badala ya Polisi Dodoma na Polisi Morogoro ambazo kuna kipindi zote zilikuwa Ligi Kuu kwa wakati mmoja.

Hivyo, kwa hili la udhamini huu wa GSM kwa timu takriban sita Ligi Kuu tunaona wadau wa soka wana hoja na TFF na Bodi ya Ligi hawapaswi kulifumbia macho kwani litaturudisha nyuma kwa kushindwa kupata bingwa aliyestahili kwa ligi yetu ambayo sasa tunatamani itoke kuwa namba sita kwa ubora Afrika na kupanda juu zaidi.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

### Wapo wanaotaka kulirudisha soka la Tanzania enzi zile za FAT

**LIGI** ya Tanzania inashika nafasi ya sita kwenye ubora wa Ligi za Afrika, na kwa sasa ina mvuto mkubwa kwa mashabiki mbalimbali duniani ambao wamekuwa wakiifuatilia.

Haikuja kwa bahati mbaya, bali kuna wadau wa soka walipambana usiku na mchana, chini ya Rais Wallace Karia kuhakikisha mpira wa Tanzania unapiga hatua.

Ligi ya Tanzania imetoka kule ambapo ilikuwa haionyeshwi kwenye televisheni, lakini kwa sasa asilimia 90 ya mechi zote zimekuwa zikionekana.

Ubora wa Ligi ya Tanzania umechangiwa na vitu vingi mno, ikiwamo viongozi wake mara kwa mara kuumiza vichwa na kuangalia wapi kunaweza kuboreshwa ili soka liwe juu.

Kuna wachezaji wengi bora wa kigeni kwa sasa ambao wameruhusiwa kuingia na kuifanya ligi kuwa na ushindani mkubwa, timu za Tanzania kufanya vema katika michezo ya kimataifa na hata wachezaji wa Kitanzania kujifunza kutoka kwao na kuikomaza Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

Binafsi hili nalipongeza na naomba viongozi washikilie msimamo huo huo, badala ya kusikiliza maneno ya watu ambao wamekuwa wakionekana kupinga sana idadi ya wachezaji 12 wa kigeni kuwapo katika kila timu.

Nadhani hii ni kwa sababu zao binafsi, labda wengi wao ni mawakala wa wachezaji wa Kitanzania, lakini hawafanyi hivyo kwa manufaa ya maendeleo ya soka la Tanzania na ligi kwa ujumla.

Lakini pamoja na hayo, bado nina wasiwasi kuwa baadhi ya mambo yanavyokwenda ni kama vile yanaanza kuturudisha nyuma enzi ya Chama cha Soka nchini (FAT), wakati kipindi hichi ni cha Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF).

Sina maana kuwa nabeza soka la kipindi hicho, la hasha, ila nyakati na kutokuwapo kwa mawasiliano bora na miundombinu ilisababisha vitu viende ndivyo sivyo. Huwezi kuwalaumu kwa sababu huwezi kupishana au kushindana na nyakati.

Nashangaa eti mpaka leo, bado kuna kesi za wachezaji kusaini timu mbili, wakati kwa wenzetu walioendelea huwezi kukuta hilo.

Ni Tanzania pekee ndiyo bado kuna kesi za wachezaji kusaini mara mbili, lakini pia Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji haitoi maamuzi, badala yake inataka klabu zilizoshindwana kwenda kuzungumza nje ya kamati hiyo.

Kamati ambayo ina hadhi sawa na ile ya FIFA kwa ngazi ya nchi, inaposhindwa kutoa maamuzi ya kesi za klabu ni ajabu kidogo. Sijawahi kusikia CAS ikirudisha kesi ya wanaopingana, badala yake inatumia sheria na kanuni ilizojiwekea kuamua. Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF, yenyewe haifanyi hivyo kwa baadhi ya kesi.

Lakini pia sijawahi kuona FIFA ilimrudisha mchezaji kwenye timu aliyoondoka kama kuna tatizo la kimkataba inamuuliza wapi anataka kucheza huku kesi ikiendelea, na yeyote atakayeonekana amekiuka taratibu anaadhibiwa, bila kuathiri mahusiano na kazi za watu.

Ukishangaa ya Mussa utaona ya Firauni, katika mechi ya Pamba Jiji dhidi ya Prisons tumesikia kuna baadhi ya wachezaji wa Pamba hawakuwa na leseni.

Katika dunia hii ya sasa kweli ligi kama hii ya Tanzania inaanza baadhi ya wachezaji kweli hawana leseni? Siku zote viongozi wa klabu na TFF walikuwa wapi? Nani mzembe kwa hili?

Kocha Goran Copunovic amelalamika sana kuhusu hilo, akadai amepanga kikosi chake, lakini kila akifanya hivyo anaambiwa kuna wachezaji hawaruhusiwi kucheza.

"Kabla ya mchezo kuna watu waliniambia TFF wamesema kuna wachezaji hawana leseni. Nikabaki na wachezaji tisa tu. Nimebadili kikosi mara tano kabla ya mchezo. Hii si sawa. Mambo ya leseni wanaohusika ni viongozi, sijui tatizo ni nini. Nitaondoka leo kama mimi ndio tatizo. Hiki ni kitu gani jamani?" akalalamika kocha huyo.

Pamoja na hayo, inadaiwa viongozi wa Prisons wamekata rufani kuwa Pamba ilichezesha wachezaji ambao hawaruhusiwi.

Jamani katika dunia hii ya leo, bado mambo haya yapo? Karne hii ya 21, kwenye Ligi Kuu ya sita kwa ubora? Nadhani kuna sehemu tumeanza kurudi nyuma enzi zile za FAT. Mbona hatujawahi kuviona huko kwenye ligi za wenzetu? Kama ni viongozi wa klabu, au ndani ya TFF waanze kuangaliana mapema kabla mambo hayajaharibika na kulitia aibu taifa.

# RITA yatoa vyeti vya vizazi, vifo kwa waombaji 195,771

**Na Kulwa Mzee**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) umepokea jumla ya maombi 198,972 ya vyeti vya vizazi na vifo katika kipindi cha miezi miwili, waombaji 195,771 (asilimia 98.4) wakipatiwa vyeti vyao.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Frank Kanyusi, alisema kuwa kati ya maombi hayo, 179,485 yalikuwa ya uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa na mengine 19,487 ni uhakiki wa vyeti vya vifo.

"Maombi mengine 18,341 yalikuwa ya upungufu uliomo kwenye vyeti hivyo ambapo wahusika walirudishiwa kwa ajili ya kufanya marekebisho, maombi 562 yalikataliwa kwa sababu vyeti vilivyowasilishwa kwa uhakiki havikuwa halali," alisema.

Kanyusi alisema maombi mengine 3,201 yanaendelea kufanyiwa kazi na yatakamilika ndani ya siku chache zijazo.

Alitaja changamoto zinazotoka kwa waombaji ni kuambatanisha nyaraka zisizo sahihi na makosa ya baadhi ya nyaraka kuwekwa nywila (password), hivyo wakala kushindwa kuzihakiki.

Akifafanua zaidi, Ofisa Mtendaji Mkuu huyo alisema kumekuwa na makosa ya kutuma nakala ya vyeti vilivyotolewa nje ya nchi ambavyo RITA haina mamlaka ya kuvihakiki sambamba na wengine kushindwa kufuatilia majibu yao ya uhakiki katika akaunti walizofungua, hivyo kuchangia ongezeko la malalamiko.

"Changamoto tulizokutana nazo zilikuwa ni nyingi lakini kwa kushirikiana na wataalamu wetu, tuliendelea kuzitafutia ufumbuzi wa haraka.

"Kwa mfano, wapo baadhi ya waombaji wamekuwa wakichagua sababu ya kuomba uhakiki tofauti na inayotakiwa ya kuomba mkopo wa elimu ya juu," alisema.

Kanyusi alisema RITA mbali ya vyeti vya uzazi na vifo, pia hupokea mombi ya wanafunzi wanaoomba vyeti vya kuzaliwa kwa ajili ya kukidhi moja ya vigezo vilivyowekwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) kupata mkopo.

Alielekeza waombaji wa mikopo ya elimu ya juu kutumia vyema muda uliobaki kuhakiki vyeti vyao vya kuzaliwa na vifo ndani ya wakati ili waweze kuwa na sifa ya kupata mikopo hiyo.

Alisema upokeaji vyeti hivyo utafungwa siku chache zijazo na hivyo kuwataka wanafunzi hao kutuma maombi yao kupitia mitandao yao kijamii ya RITA ili waweze kujua vigezo vya kukidhi maombi yao.



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuph Mwenda (aliyesimama kulia), Waziri wa Mamlaka ya Forodha ya Jamhuri ya Watu wa China, Yu Jianhua (aliyesimama kushoto), wakishuhudia utiaji saini wa kukuza uhusiano baina ya Tanzania na China katika masuala ya forodha. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# PBZ yaongeza faida kwa asilimia 18 katika nusu ya kwanza ya 2024

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Watu wa Zanzibar (PBZ) imetangaza ripoti yake ya kifedha ya nusu ya kwanza ya mwaka 2024, ikionesha mafanikio katika nyanja mbalimbali, likiwamo ongezeko la faida ya jumla baada ya kodi kwa asilimia 18.

Ikiashiria maendeleo mazuri ya benki hiyo, ripoti hiyo inaonesha ongezeko la mapato hadi kufikia Sh. bilioni 31.15 (ikiwa ni faida kabla ya kodi Sh. bilioni 44.50).

Kiasi hicho kinawakilisha ongezeko la asilimia 18 kulinganisha na kipindi kama hicho mwaka jana, ikithibitisha uwezo wa benki hiyo katika kuendesha ukuaji endelevu na faida.

Mafanikio hayo yamechagizwa na ongezeko la mapato yatokayo na riba (Net Interest Income) ya benki hiyo ambayo yamefikia Sh. bilioni 54.15, ikiwa ni ongezeko la asilimia 14 kulinganishwa na mwezi Juni mwaka 2023.

Mafanikio haya yanatajwa kama ushahidi wa utekelezaji mzuri wa mikakati ya benki, kwa mujibu wa Mkurugenzi Mwendeshaji wake, Arafat Haji.

"Ukuaji huu ni ushahidi wa utekelezaji mzuri mikakati yetu ambayo ililenga kuongeza rasilimali zetu kwa kuboresha usimamizi na ufanisi wa muundo wa kitabu chetu cha mizania (balance sheet), tukisaidiwa na huduma bora kwa wateja wetu, na azma ya timu ya wafanyakazi wetu katika kutimiza ahadi zetu kwa wateja na wadau wetu," alisema Haji kupitia taarifa ya benki hiyo iliyotolewa kwa vyombo vya habari mwishoni mwa wiki.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mwendeshaji huyo, mafanikio hayo kwa kiasi kikubwa yametokana na sera imara za kiuchumi zinazolenga kuchochea uwekezaji na ukuaji wa biashara, zinazotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais Hussein Ali Mwinyi.

Alisema benki hiyo imeendelea kudhihirisha dhamira yake ya uendeshaji wenye ufanisi ambapo uwiano wake wa gharama za uendeshaji na mapato (cost-to-income ratio) ulikuwa asilimia 46.49, kiasi ambacho hakijavuka matakwa ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) yanayoelekeza kiwango hicho kisizidi asilimia 50.

Ufanisi wa benki hiyo hauishii kwenye matokeo yake ya kifedha bali pia unathibitishwa na ongezeko kubwa la rasilimali zake ambapo jumla yake imeongezeka hadi kufikia thamani ya Sh. trilioni 2.23, ikiwa ni ongezeko la asilimia 22 kutoka Sh. trilioni 1.83 iliyoripotiwa mwezi Juni mwaka 2023.

Zaidi, mwenendo wa mikopo wa benki hiyo umekua hadi kufikia Sh. trilioni 1.11 kutoka Sh. bilioni 932 iliyoripotiwa mwezi Juni 2023, huku msingi wa amana ukishuhudia ongezeko kubwa la asilimia 31 ambapo umefikia kiasi cha Sh. trilioni 1.77.

Akitoa maoni kuhusu ukuaji huo, Haji alisema: "Ukuaji huu unaonesha imani ambayo wateja wetu waliweka kwetu na uwezo wetu wa kukidhi mahitaji yao ya kifedha na kuwapa suluhisho za kusaidia mahitaji yao."

Ubora wa mali (asset quality) wa benki hiyo ulibaki kuwa imara zaidi huku kiwango cha mikopo chechefu kikiwa ni asilimia 2.44 tu, ikiwa ni chini ya kiwango cha asilimia tano kilichowekwa na BoT.

Hatua hiyo inatajwa kudhihirisha uimara wa usimamizi na utambuzi wa hatari kwenye utoaji mikopo .

Pamoja na mafanikio yake ya kifedha, benki hiyo pia imepiga hatua katika kuongeza kuwapo kwake kidijiti na kuongeza matawi yake nchini.

Hivi karibuni, benki hiyo ilifungua matawi yake mapya katika mikoa ya Morogoro na Mbeya huku ikiongeza idadi ya mawakala wake hadi kufikia 114, lengo likiwa kuimarisha zaidi upatikanaji na ufikiwaji wake kwa wateja kote nchini.

"Zaidi ya hayo, programu yetu ya simu (Mobile App) imefanyiwa maboresho makubwa na sasa wateja wanaweza kuipata kupitia simu zao za aina zote ikiwa ni azma yetu ya kutoa uzoefu wa kihuduma usio na dosari za kiteknolojia," aliongeza Haji.

Akizungumzia mipango ijayo, Haji alisema benki hiyo itabaki kuwa imara katika jitihada zake za kuimarisha nafasi yake katika soko na kuzidi malengo yake kwa mwaka 2024.

Alisema wataendelea kuangazia na kuboresha uzoefu na kuridhika kwa wateja, wakiboresha zaidi uwekezaji wao katika teknolojia ili kuchochea uvumbuzi na kuendeleza muundo wa kitabu cha mizania imara ili kufanikisha ukuaji endelevu.

"Tuna uhakika kwamba tuko katika nafasi nzuri ya kufikia malengo yetu ya baadaye. Ninatoa shukrani zangu kwa wafanyakazi wenzangu wote katika benki kwa kazi yao nzuri miaka yote.

"Juhudi zao zimekuwa ni za kutia moyo sana na ndio sababu ya matokeo mazuri na ukuaji unaodumu wa benki, na tuna uhakika kwamba tuko katika nafasi nzuri ya kufikia malengo yetu ya baadaye," alipongeza.

Vilevile, kiongozi huyo alishukuru wateja na wadau wa benki hiyo kwa msaada wao endelevu katika ukuaji na maboresho makubwa ya benki.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Korti Kuu kutoa uamuzi kesi ya Msajili wa Hati, wenzake

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Divisheni ya Ardhi, Septemba 6 mwaka huu inatarajiwa kutoa uamuzi wa pingamizi lililowasilishwa na upande wa serikali katika kesi ya mgogoro wa uhamisho wa ardhi iliyofunguliwa na Kampuni ya Nicoland dhidi ya Msajili wa Hati na wenzake watatu.

Mawakili wa serikali wamewasilisha taarifa mahakamani kwamba ardhi iliyoko eneo la Kigamboni (Kimbiji), mkoani Dar es Salaam yenye hati namba 124963 ilitwaliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hoja ambayo ilionekana kuwa si ya kweli.

Uamuzi huo unatarajiwa kutolewa na Jaji Dk. Theodora Mwenegoha baada ya pande zote kuwasilisha mahakamani huko hoja zao kwa njia ya maandishi kutokana na hoja zilizoibuka katika usikilizwaji kesi hiyo zinazohusiana na uhamishaji hati ya eneo hilo.

Mbali na Msajili, wadaiwa wengine ni Kamishna wa Ardhi, Taasisi ya Tanzania Housing Business Company (THBC) na Manispaa ya Kigamboni.

Ilidaiwa kuwa mwaka 2022, Kampuni ya Nicoland ilifikia hatua ya makubaliano ya kununua ardhi katika eneo la Kigamboni (Kimbiji), Dar es Salaam kwa lengo la kujenga kiwanda cha mabati.

Ardhi hiyo yenye hati namba 124963 inadaiwa ilikuwa ikimilikiwa na Balthazar Kitundu. Baada ya ununuzi kukamilika, taratibu za kisheria zilikamilishwa ikiwa ni pamoja na kulipwa kwa kodi ya stempu Sh. 45,660,000 na kodi ya mapato ya mtaji (capital gain tax) Sh. 218,164,000.

Hatua hiyo inadaiwa ilitarajiwa kufanikisha kubadilisha umiliki wa ardhi hiyo kwenda kwa jina la Nicoland ili kuwezesha kuendelea na mradi huo.

Hata hivyo, ilidaiwa kuwa mchakato wa usajili wa ardhi hiyo ulichukua muda mrefu, kinyume cha matarajio ya Nicoland licha ya mawasiliano kadhaa na Msajili wa Hati na Kamishna wa Ardhi, Nathaniel Mathew.

"Hili lilichukua sura mpya mara baada ya Msajili wa Hati kutoa taarifa za nia ya kurejesha hati hii THBC ambayo haitambuliki popote katika umiliki wa ardhi hiyo na hakuwa mmiliki halali wa ardhi," Nicoland inadai katika hati yake ya madai. Ilidaiwa kuwa katika uchunguzi wa Nicoland, ilibainika kuwa taasisi hiyo haikuwa hai na wamiliki wake walijumuisha John Chagama na Philip Mangula ambao hata hivyo walikanusha kuwa na maslahi yoyote ya kuzuia uhamisho wa ardhi hiyo.

Kampuni ya Nicoland ilifungua shauri namba 26386 mwaka 2023 dhidi ya Msajili wa Hati, Kamishna wa Ardhi, THBC na Manispaa ya Kigamboni na kufanikiwa kutolewa zuio Desemba Mosi, 2023 lililotolewa na Jaji Lusungu Hemed katika kesi ya ardhi namba 5294 ya mwaka 2024 inayoendelea Mahakama Kuu.

Wahusika wa Nicoland na THBC walikubaliana kutatua suala hilo kwa njia ya makubaliano.

Hata hivyo, mawakili wa serikali waliwasilisha taarifa kwamba ardhi hiyo ilitwaliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hoja ambayo ilionekana kuwa si ya kweli baada ya ushahidi wa matokeo ya utafutaji hati kuonesha kuwa mmiliki halali ni Bartzaar Kitundu.

# Machifu kuhamasisha wananchi kupiga kura

**Na Halfani Chusi**

KIONGOZI Mkuu wa Jamii ya Kimasai Tanzania, Laigwanan, Isack Kisongo, ameelekeza machifu wa jamii hiyo waliosimikwa juzi, kuhamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapigakura pamoja na kupiga kura kuchagua viongozi bora.

Hafla hiyo ya kuwasimika machifu hao watano watakaotoa huduma katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, ilifanyika jijini hapa na ilihudhuriwa na jamii ya Wamasai kutoka mikoa mbalimbali na viongozi wa dini.

Akizungumza wakati wa kuwasimika kiongozi huyo, Kisongo alisema kuna tabia imejengeka miongoni mwa watu kuwa kushiriki uchaguzi na kujiandikisha kupata kadi ya mpigakura ni kupoteza muda, jambo ambalo si kweli.

"Ninyi viongozi mliosimikwa leo, sisi wazee tunawategemea kwenda kuhamasisha jamii kujiandikisha katika daftari la maboresho, ili kupata kadi itakayomsaidia kupiga kura na kuchagua kiongozi anayemtaka.

"Mtu asiishie kujiandikisha tu, bali ashiriki kupiga kura katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu kwani kufanya hivyo ni kuliletea maendeleo taifa letu," alisema.

Kisongo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Umoja wa Jamii ya Wamasai nchini, alisema matatizo katika ndoa hayaepukiki, akisisitiza jambo la msingi ni kukaa chini kuangalia ni namna gani ya kumaliza migogoro na si kukimbilia nyumbani; kufanya hivyo kunapunguza heshima ya familia.

Mwenyekiti wa Machifu Tanzania, Antonia Sangalali alisema ni wakati wa kuenzi mila kwa kuwa kupitia Wamaasai, watalii wengi wanakuja nchini kwa ajili ya kufanya utalii, jambo linaloongeza na kukuza Pato la Taifa.


TOL Gases PLC since 1950 We Deliver

Plot 4B, Nyerere Road, P. O. Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, E – mail: info@tol-gases.co.tz

## TAARIFA

## MKUTANO WA 29 WA WANAHISA WOTE

**TAARIFA INATOLEWA HAPA** kuwa Mkutano Mkuu wa 29 wa Wanahisa wote wa TOL Gases PLC utafanyika kwenye ukumbi wa Mlimani City Dar es Salaam na kwa njia ya mtandao wa ZOOM, siku ya tarehe 29 Agosti 2024, kuanzia saa 3.00 asubuhi kufanya shughuli zifuatazo:-

1. Kuikubali Ajenda.
2. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano wa 28 wa Wanahisa. uliofanyika tarehe 25 Agosti, 2023.
3. Yatokanayo na Kumbukumbu za Mkutano wa 28 wa Wanahisa.
4. Taarifa ya Mwenyekiti.
5. Kupokea Ripoti ya Wakurugenzi, Ripoti ya Wakaguzi wa Mahesabu na Mahesabu yaliyokaguliwa kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2023.
6. Malipo ya Gawio.
7. Kuidhinisha Ada za Wakurugenzi.
8. Kuteua Wakaguzi wa Mahesabu kwa mwaka 2024.
9. Kuteua Wakurugenzi.
10. Kupanga sehemu na tarehe ya Mkutano Mkuu wa 30 wa Wanahisa.
11. Mengineyo (yaliyotaarifiwa rasmi angalau siku saba kabla ya mkutano).

Kujisajili ili kushiriki mkutano kwa njia ya mtandao kutafanyika kupitia namba **0685750201/0685750203**

Mwanahisa anayestahili kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano huu anaruhusiwa kuteua mtu mwingine (awe Mwanahisa wa Kampuni au la) kuhudhuria na kupiga kura badala yake.

Fomu zote za uwakilishi (proxy forms) ama barua za kuteua wawakilishi zifikishwe katika ofisi ya Katibu wa Kampuni angalau saa 48 kabla ya muda uliopangwa kufanyika mkutano au kupitia email **mjuliana@tol-gases.co.tz / nlulu@tol-gases.co.tz**

**KWA AMRI YA BODI YA WAKURUGENZI.**

**CORNELIUS KASIYA KARIWA**

Directors: H. Kitilya – Chairperson (Tanzanian), T. Kinabo - (Tanzanian), J. Massawe – (Tanzanian), L. Kitoka (Tanzanian) S. Selestine – TR - URT (Tanzanian), Prof. A. Temu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzanian)



TAMBAZA AUCTION MART & GENERAL BROKERS LIMITED

## TAMBAZA AUCTION MART & GENERAL BROKERS LIMITED
## MARUDIO YA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini niliyopewa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (N.S.S.F MAKAO MAKUU) nitauza kwa mnada wa hadhara vitu/mali za wadaiwa wa NSSF kama ilivyoonyesha kwenye jedwali hapa chini: -

| NA. | MDAIWA | MALI HUSIKA | MNADA UTAKAPOFANYIKA | TAREHE | SIFA ZA MALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | MSAJIGWA JOAB ULISAJA NA KYEMBE DITOPILE MZUZURI | SAMANI ZA MAJUMBANI | SINZA MORI TAMBAZA MAKAO MAKUU | 26/08/2024 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | SOFASET, VITANDA, MAGODORO, FRIJI, MEZA, TV,REDIO, NA VITU VINGINE VINGI. |
| 2. | MOHAMEDH ARRI SAID | SAMANI ZA MAJUMBANI | TEMESA | 27/08/2024 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | SOFASET, VITANDA, MAGODORO, FRIJI, MEZA, TV,REDIO, NA VITU VINGINE VINGI |
| 3. | TANZANIA DAR COACH | BODI LA BASI NA VITU VIDOGO | HIFADHI ENEO LA UZALISHAJI KWAAJILI YA MAUZO NJE YA NCHI (HEPZ) | 27/08/2024 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | BODI LA BASI KUBWA PAMOJA NA VITU VINGINE VIDOGOVIDOGO |
| 4. | DEIGU COMPANY LIMITED | SAMANI ZA OFISINI | KIIJMANJARO COMMERCIAL CONFERENCE | 31/08/2027 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | 1. NGUO ZA KIUME, 2. VIATU, 3. MIDOLI YA KUVISHA NGUO ZA KUUZA, 4. UBAO WA MATANGAZO, 5. REDIO N.K |
| 5. | ANGELA KESSY | VITU VYA DUKANI/ NGUO TOFAUTI | KIIJMANJARO COMMERCIAL CONFERENCE | 31/08/2027 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | 1. NGUO ZA KIUME, 2. VIATU, 3. 4. MIDOLI YA KUVISHA NGUO ZA KUUZA, 5. UBAO WA MATANGAZO, 4. REDIO N.K |
| 6. | GRIENFIN | VITU VYA BAR | KIIJMANJARO COMMERCIAL CONFERENCE | 31/08/2027 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | VITI, MEZA, TV, MAJIKO,FRIJI, MUSIC SYSTEM N.K |
| 7. | LEO NYAKI | VITU VYA STATIONARI | KIIJMANJARO COMMERCIAL CONFERENCE | 01/09/2024 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | PHOTOCOPY, PRINTER, MEZA YA KIOO, N.K |
| 8. | NORTHERN SAVING AND CREDIT COOPERATIO N | SAMANI ZA OFISINI | KIIJMANJARO COMMERCIAL CONFERENCE | 01/09/2024 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | PRINTER, C.P.U,SAFEYA KUWEKEA VITU VYA THAMANI, PHOTOCOPY MASHINE,MEZA NA VITU VYA OFISINI N.K |
| 9. | VERYNICE | VINYWAJI NA VITU VYA BAR | KIIJMANJARO COMMERCIAL CONFERENCE | 01/09/2024 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | MUSIC SYSTEM, VINYWAJI, TV, MAJIKO, VITU, MEZA. FRIJI |
| 10. | UPENDO ASUKENYE KIBONA | SAMANI ZA OFISINI | ARUSHA– MAFAO HOUSE | 02/09/2024 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | SAMANI HIZO NI PAMOJA NA ZA OFISINI NA VITU VYA DUKANI |

**MASHARTI YA MNADA**

Mnunuzi atatakiwa kulipa 100% ya vitu kama fenicha au vitu vyote vidogo vidogo visivyozidi milioni moja ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi.

Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya kiasi alichobidi ambacho kinazidi zaidi ya milioni moja na salio la 75% ni lazima alipe ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya mnada. Kiasi cha 25% kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio la 75% katika kipindi cha siku 14 kuanzia tarehe ya mnada.

i. Gharama zote za kutoa vitu vilivyouzwa ni jukumu la mteja mwenyewe.
ii. Mshindi atakakabidhiwa Mali/Kitu/Vitu mara baada ya kufanya malipo kamili (100%).
iii. Ukaguzi ni siku moja kabla ya tarehe ya mnada.

**KWA MAELEKEZO ZAIDI PIGA SIMU 0713 – 327 989/ 0713 508 158 AU BARUA PEPE; info@tambazaauctionmart.co.tz AU FIKA OFISINI KWETU SINZA MORI, BARABARA YA SHEKILANGO KARIBU NA KITUO CHA MAFUTA BI**



# Diwani alalama milioni 20/- kutojenga zahanati ya kijiji

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

DIWANI wa Naisinyai wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Taiko Laizer, amefikisha malalamiko kwa mbunge wa jimbo hilo, Christopher Ole Sendeka, kuhusu kutokutumika kwa Sh.milioni 20 zilizotengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa zahanati.

Fedha za ujenzi wa zahanati hiyo iliyopo Kijiji cha Naepo wilayani humo zimetolewa na mwekezaji, kwamba inadaiwa zimeshidikana kutumika kutokana na kuwepo kwa tatizo la kimfumo.

Aliwasilisha malalamiko hayo juzi wakati wa ziara ya Ole Sendeka, iliyolenga kusikiliza kero na kuelezea mafanikio ya miradi mbalimbali.

Diwani huyo alisema mwekezaji ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Franone Mining Ltd, Onesmo Mbise, aliwapatia Sh. milioni 20 kwenye akaunti ya Kijiji cha Naepo ili wakamilishe ujenzi wa zahanati, lakini wamekwamishwa kwa madai kuwa mfumo hausomi.

"Tulitarajia kukamilisha Zahanati ya Kijiji cha Naepo kupitia fedha hizo za mwekezaji ambazo aliweka kwenye akaunti ya kijiji, ila tunapigwa danadana kuwa mfumo hausomi," alisema diwani huyo.

Hata hivyo alisema wananchi wanacheleweshewa maendeleo kwa kuwa fedha hizo ziliwekwa kwa ajili ya kazi hiyo na inapaswa utekelezaji wake uendelee na sio kukwamishwa na mfumo.

Alisema: "Wanatuandalia mazingira mabaya ya kutuhoji kuwa tumeshindwa kutumia fedha zilizopo kwenye akaunti, hivyo hatupaswi kupewa fedha nyingine, hivyo suala hili linatakiwa lishughulikiwe mapema wananchi wasivunjwe moyo na wapate maendeleo."

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Baraka Kanunga, alimhakikishia diwani huyo kuwa atalifuatilia suala hilo kwa kuwa wakati mwingine mfumo wa fedha unakuwa na changamoto ifikapo mwanzo wa mwaka wa fedha.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Simanjiro, Kiria Laizer, aliwaagiza Ole Sendeka, Kanunga na Taiko, kufuatilia ujenzi wa barabara fupi ya kutoka Emishiye hadi Lengasiti.

Aidha, Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa, kupitia Wilaya ya Simanjiro, Lenganasa Soipey, aliwapongeza wananchi wa eneo hilo kwa kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Akizungumza na wananchi, Ole Sendeka, alisema wamefanikiwa kujenga zahanati kwenye kila kijiji katika Kata ya Naisinyai na kupeleka nishati ya umeme kwenye vijiji vyote vitano.

Alisema: "Maji tumefikisha maeneo yote, sasa tutahakikisha minara ya mawasiliano ya simu inakuwapo na Barabara ya Emishie hadi Lengasti na Emishie hadi Landanai, inafunguka kuliko kuzungukia Mirerani".

Aidha alisema utekelezaji wa miradi hiyo ya maendeleo inatokana na uwezeshaji wa serikali chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

## Marekani yatoa mil.250/- kusaidia wakulima kahawa

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

SERIKALI ya Marekani kupitia Taasisi ya Maendeleo ya Afrika ya US African Development Foundation (USADF), imetoa ruzuku ya Sh. milioni 250 kwa Chama cha Ushirika wa Wakulima wa Lukani/Losaa Amcos Limited.

Fedha hizo ni kwa ajili ya kutatua changamoto zinazoathiri ongezeko la uzalishaji wa kahawa maalum inayokwenda moja kwa moja katika soko la nje ya nchi.

Chama hicho chenye wanachama 580 kilichoko Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, kinatekeleza mpango mkakati wa miaka mitano (2024/2029).

Mkakati huo unalenga kuongeza uzalishaji kwa kuhamasisha wakulima wapya na upanuzi wa mashamba, kuweka mfumo wa kidijitali wa kuweka na kutunza taarifa za biashara na hesabu za chama.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, Mratibu Mkazi wa Miradi wa USADF nchini Tanzania, Gilliard Nkini, alisema taasisi hiyo inashirikiana na Serikali ya Tanzania kuongeza tija kwenye sekta ya kahawa.

Nkini alisema: "Tunajua kabisa kwamba ili nchi ya wakulima iweze ikapata tija na mkulima akapata tija na kufaidika kikweli kweli, ni lazima wajiunge kwenye vikundi vya ushirika na viwe vinasimamiwa kwa karibu na Mrajis wa Vyama vya Ushirika".

Aliongeza: "USADF iko kwenye nchi 22 za Afrika, ikiinua kipato cha wakulima na wasindikaji wa mazo ya kilimo, ikijua kwamba hapo ndipo uchumi wa nchi za Afrika ulipo."

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Chama cha Lukani/Losaa Amcos Limited, Ebenetho Munuo, alisema upatikanaji wa ruzuku hiyo umetokana na chama hicho kuwa na mpango mkakati na thabiti wa uendelezaji wa kahawa kwa mfumo wa ushirika.

Alisema: "Masharti makubwa ya ruzuku hii ni kuelekeza fedha za mradi kwenye ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji na uchakataji wa kahawa, kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, uhifadhi wa mazingira, kuimarisha mifumo ya kutoa maarifa na taarifa muhimu kuhusu uzalishaji bora na wenye tija".

Alisema lengo la jumla la mradi ni kuongeza wingi wa ubora wa kahawa, bei ya kahawa na kipato kwa mkulima na hatimaye kuongezeka kwa ubora wa maisha kwa wakulima wa kahawa na jamii kwa ujumla.

Alisema makisio ya msimu wa mwaka 2025/26 ni kuvuna kahawa kilogramu 150,000.

Aidha, kulingana na taarifa za chama hicho, fursa za masoko ya nje zimeongezeka na sasa wana soko la moja kwa moja nchini Japan, Marekani, Australia na China tayari imeonyesha nia ya kununua kahawa yao katika msimu ujao.

## Wakazi vijiji Losinyai, Einot kufikiwa na mradi wa maji

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WAKAZI wa vijiji vya Losinyai na Einot katika Kata ya Oljoro Namba Tano wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wanatarajia kufikiwa na huduma ya majisafi na salama, baada ya Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kuanza kusambaza mabomba.

Diwani wa kata hiyo, Loishiye Lesakwi alisema wananchi wa eneo hilo wanashukuru kwa uwekaji wa mabomba hayo ili kuendeleza mradi wa maji.

Aidha, alisema mradi huo wenye thamani ya Sh.milioni 383 ukikamilika utanufaisha wakazi wa vijiji vya Losinyai na Einot pamoja na mifugo ya eneo hilo.

Alisema mtandao wa mabomba ukishafungwa kwenye mradi utafikia asilimia 67 na wanatarajia utakamilika hivi karibuni na jamii kuanza kutumia maji.

Hivyo, aliishukuru serikali kwa kuwapambania wananchi wa kata hiyo kwa kutoa fedha za kufanikisha ujenzi wa mradi huo.

"Tunawashukuru RUWASA Mkoa wa Manyara na Wilaya ya Simanjiro kwa kuendelea kufanya kazi kubwa na nzuri na tunatarajia usambazaji wa mabomba yatafika eneo la mradi na kuanza kufungwa kwa ajili ya kukamilisha mradi," alisema Lesakwi.

Alisema baada ya mtandao wa mabomba kuanza kusambazwa kwenye maeneo yaliyobaki jamii na mifugo watapata fursa ya kunufaika na maji hayo.

"Mabomba yamefika ila tunawaomba yafungwe kwa kuwa ni kazi kubwa RUWASA wamefanya, hivyo tunasubiria matokeo mazuri kupitia mradi huu," alisema Lesakwi.

Pia, alisema wakala hao kupitia kauli mbiu yao ya 'maji bombani', wanatarajia wananchi hao, watanufaika na mradi huo hivi karibuni, kwamba endapo ukikamilika italeta ukombozi kwa wananchi.

Mkazi wa Kijiji cha Losinyai, Sinyati Lazaro, aliishukuru RUWASA kwa kufikisha mabomba ya maji, ambapo alieleza kuwa ilikuwa ni ndoto yao ya muda mrefu ya kupata maji na itatimia.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA MWANZA NA SHINYANGA**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza mzunguko wa tatu unaanza kufanyika tarehe 21 hadi 27, Agosti, 2024 katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga kwa siku saba kwa kila kituo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Jumatano tarehe 21 na kuhitimishwa Jumanne tarehe 27 Agosti, 2024.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 9 na kubonyeza.Kisha atachagua Namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

***KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***

**Limetolewa tarehe 16 Agosti, 2024 na:**

**Kalima, R. K.**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**



# Mwenge wa Uhuru wamulika shamba la miti

**Na Mwandishi Wetu,** TABORA

KAMPUNI ya ununuzi wa tumbaku ya Alliance One imeanza kurejesha misitu ya asili iliyoharibiwa na shughuli za kibinadamu kwa kupanda miti 1,062,500, katika mradi wa shamba la miti la Ngukumo wilayani Nzega mkoani Tabora wenye thamani ya Sh. milioni 980.

Msimamizi mkuu wa misitu wa kampuni hiyo, Rashid Salum, alisema hayo wakati Mwenge wa Uhuru ulipotembelea shamba hilo.

Alisema hatua hiyo ni mwendelezo wa mkakati wa kampuni hiyo kupanda miti katika maeneo mbalimbali kunakozalishwa tumbaku ambako walianza Kasulu Mkoa wa Kigoma mwaka 2014 ambako waliopanda miti katika hekta 450.

Alisema waliingia mkataba wa makubaliano na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega wa kuanzisha mradi wa upandaji miti kwa umiliki kwa mkataba wa Alliance One kumiliki asilimia 80 na Halmashauri ya Nzega kumiliki asilimia 20.

Alisema mradi ulianza Desemba 2022/23 kwa kusafisha eneo, kuchimba mashimo na kupanda miti aina ya mfudufudu au mitiki myeupe.

Alisema wanaprogramu tatu za uzalishaji miti ambapo ya kwanza wanawahamasisha wakulima kupanda miti katika maeneo yao kwa ajili ya kukaushia tumbaku badala ya kukata miti ya asili ambayo kwa sehemu kubwa imesababisha uharibifu wa misitu.

Alisema programu ya pili ni wakulima wanapandiwa miti na kampuni kwa kuwagharamia mpaka asilimia 40 katika mashamba ya pamoja na programu ya tatu ni ya ushirikiano ambayo kampuni inaanzisha shamba na kupanda miti.

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru, Godfrey Mnzava, alisema ili shughuli za kilimo cha tumbaku ziweze kuwa endelevu ni lazima ziende sambamba na upandaji miti ya kukaushia zao hilo.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, Maria Katema, alisema shamba hilo litarejesha misitu iliyoharibiwa na shughuli za kibinadamu.

Katema alisema eneo lililopandwa miti lilikuwa msitu mkubwa, lakini uliharibiwa na shughuli za kibinadamu zikiwamo utengenezaji mkaa.



Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Godfrey Mzava (katikati), akikata utepe kwenye shamba la miti lililoko Kijiji cha Ngukumo, Kata ya Nkikizwa wilayani Nzega, mkoani Tabora, wakati msafara wa Mwenge ulipotembelea shamba hilo lililopandwa na kutunzwa na Kampuni ya Alliance One kwa ajili ya matumizi ya wananchi. Baadhi ya wanaoshuhudia tukio hilo ni Msimamizi wa Miti wa Kampuni hiyo, Salum Rashid (wa tano kulia) na Mbunge wa Nzega Vijijini, Hamis Kigwangallah (mwenye shati la kijani). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi wachekelea kurejeshwa ukokotoaji hisabati

**Na Restuta Damian,** KAGERA

SERIKALI imefanya uboreshaji katika elimu kwa kufanyia mabadiliko ya masomo kwenye shule za msingi, kwa kurejesha ukokotoaji katika somo la hisabati ikiwa na lengo la kutoa fursa kwa wanafunzi kujifunza kwa njia ya vitendo na kutumia maarifa.

Mwaka 2015 serikali ilibadili mfumo wa kujibu mitihani ya hesabu kwa kuja na utaratibu wa kuchagua ili kupata jibu hasa katika somo la hisabati, mfumo huo ulikuwa unatoa maudhui ya kinadharia bila kuzingatia uwezo wa mwanafunzi.

Hatua hiyo inatajwa kuwafanya wanafunzi kukosa uelewa na kutowajibika kwenye ufanisi wa somo hilo, kwamba waliweza hata kufanya inavyowezekana ili kukamilisha somo hilo.

Wakizungumza na Nipashe iliyofika katika Shule ya Msingi Rumuli iliyopo Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera na kujionea hali ya mapokeo ya wanafunzi wanaotarajiwa kufanya mitihani ya kuhitimu darasa la saba.

Baadhi ya wanafunzi walieleza kuwa hatua hiyo huwasaidia katika uelewa tofauti na utaratibu wa awali.

Mwanafunzi wa darasa la saba, Tunukio Kennedy alisema, serikali imesaidia kuondoa mfumo huo na kurudisha ule wa kukokotoa hali inayoleta matumaini na kuwasaidia wanafunzi kuelewa wanachokifanya wakati wa mtihani.

Aidha, alisema awali ilikuwa vigumu kujua jibu sahihi ni lipi kwa ilikuwa ni kubahatisha, hivyo ilibaki kuwa hofu ya kwamba amepata au amekosea lakini sasa inawafanya kujiamini.

Alisema kupima uelewa wa mwanafunzi ni kupitia njia anayotumia katika kanuni alizopewa na walimu wake katika vipindi.

Mwanafunzi mwingingi wa darasa la saba, Joram Ijumba alisema uelewa unapatikana katika kufanya swali na kupata jibu ambalo linaulizwa kuliko lile ambalo limewekwa katika kuchagua.

Mwalimu wa Somo la Hisabati shuleni hapo, Philemon Faustine, alisema jibu la hisabati linategemea ukokotoaji na wanafunzi wanakuwa huru wakifanya njia ya kutafuta jibu.

Alisema: "Mfumo wa sasa unasaidia wanafunzi kwani amejibu kila ambacho amefundishwa na mwalimu darasani na kwa umri wa hawa watoto wa shule ya msingi wanaamini walichofundishwa".

# Wananchi Tarime wapewa hadhari utapeli viwanja

**Na Samson Chacha,** TARIME

HALMASHAURI ya Mji wa Tarime mkoani Mara imewataka wananchi kuepukana na watu wanaodaiwa ni matapeli wanaopita mitaani wakisema wanauza viwanja.

Imesema watu hao wanatangaza kuuza viwanja hasa katika maeneo yasiyoruhusiwa ikiwamo Soko la Bomani.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Gwambina Ntovya, wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake baada ya kutokea kwa uvumi wa kuwapo viwanja zaidi ya 300 vinavyotolewa na halmashauri hiyo kwa ajili ya shughuli za biashara sokoni hapo.

"Kumekuwa na tetesi tuna mpango wa kugawa viwanja zaidi ya 300 vilivyopo katika maeneo ya Msitu wa Bomani kutoka darajani, maeneo yanayozunguka Hospitali ya Wilaya na Chuo cha Veta, huku wengine wakidai kuwa watu walishapewa vibanda katika soko kuu linalotarajiwa kukamilika wakati wowote," alisema Ntovya.

Alisema taarifa hizo ni za uzushi, kwamba hakuna ugawaji wa viwanja uliofanyika wala unaoendelea kwa sasa mpaka pale wakati utakapofika.

Alisema ugawaji ukianza taarifa itatolewa katika Gazeti la Serikali na wananchi waliokuwa na vibanda katika soko hilo hapo awali ndiyo watapewa kipaumbele.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Daniel Komote, akizungumza na Nipashe aliwataka wananchi kuepukana na vishoka wanaopita mitaani kutaka kupewa fedha kwa ajili ya kuwafanyia mipango ya kupata viwanja.

Aidha, aliwataka wote wanaokutana na watu wa namna hiyo kuhakikisha wanatoa taarifa katika vyombo husika ili wachukuliwe hatua za kisheria.

# Madiwani wakerwa mrundikano taka katika makazi

**Na Timothy Itembe,** TARIME

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Tarime Mji limeitaka halmashauri hiyo kupitia Ofisa Afya wa Wilaya, Erasto Mbunga, kuhakikisha wanatumia Sh. milioni 20 zilizotengwa kwa ajili ya kuhamisha 'dampo' lililopo katika Kata ya Nyamisangura.

Madiwani hao wamesema dampo hilo liende Kata ya Nkende eneo la Magena, kuanza kutumika ili kuondoa kero ya uchafu katika makazi ya wananchi.

Walitoa agizo hilo juzi katika kikao cha robo ya nne ya mwaka 2023/2024 kilichoongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Daniel Komote, ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Nkende.

"Tusidanganyane katika vikao vyetu hali ya mazingira maeneo mengi ni mbaya, taka zimekuwa nyingi sababu hazizolewi kwa wakati, hivyo ifike hatua halmashauri itangaze tenda kazi hiyo ifanywe na wengine kuliko kumtegemea Ofisa Afya tu na gari lake moja la kuzoa taka," alisema Kamote.

Aidha, alisema kutokana na hali ya mazingira kuzidi kuwa mbaya baraza hilo limekubaliana kwa pamoja kumpa siku saba ofisa huyo kuhakikisha dampo la Mwangaza linahamishwa ili kuepukana na magonjwa ya mlipuko.

Katika hatua nyingine, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) Kanda ya Tarime, chini ya Mkurugenzi Mtendaji, Nicas Mugisha, imesema imeandaa mipango mitatu ya kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Tarime.

Nipashe
# Spotika



MAKINDA 11 WA KUTAZAMWA LIGI KUU ENGLAND MSIMU HUU UK. 12




Mo Salah akiifungia timu yake katika mechi ya kwanza ya msimu huu dhidi ya Ipswich Town wakati Liverpool ikishinda mabao 2-0 juzi. **PICHA: MTANDAO**

Activate Windows

# WACHEZAJI WA AFRIKA NA MATARAJIO ENGLAND

**LONDON, England**

BAADA ya kipindi chenye shughuli nyingi cha michuano ya Ulaya, Copa America na Olimpiki, sasa mashabiki wa soka barani Afrika kwa mara nyingine tena wanaelekeza macho yao kwenye Ligi Kuu England, EPL.

Msimu mpya ulianza Ijumaa pale Manchester United walipowakaribisha Fulham kwenye dimba la Old Trafford.

Mshambuliaji wa Senegal, Iliman Ndaiye, winga wa Ghana Ibrahim Osman na mlinzi wa Morocco, Chadi Riad ni miongoni mwa wachezaji wapya wa Afrika waliojiunga na ligi hiyo inayofuatiliwa zaidi duniani.

Makala haya yanajadili baadhi ya maswali makubwa ambayo yatajibiwa katika kipindi cha miezi tisa ijayo.

### Salah atakuwa na jipya?

Mohamed Salah ni moja ya wachezaji bora kutoka Afrika kuwahi kuingia katika Ligi Kuu England. Nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya Misri, hakuwa katika ubora wake katika msimu uliopita, aliporomoka mwishoni mwa msimu huku Liverpool ikishindwa kutwaa taji la ligi hiyo.

Mabao yake 18 katika Ligi Kuu England - matano kati ya hayo yalitokana na mikwaju ya penalti - ni kiwango cha chini kabisa cha mabao tangu ajiunge na Liverpool mwaka 2017, ingawa pia alitoa asisti 10.

Jeraha lilimfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, kukosa mechi nyingi za Kombe la Mataifa ya Afrika 2023, pamoja na mechi kadhaa za nyumbani, na tatizo lilionekana kuzidi Aprili pale alipoingia katika mzozo na kocha Jurgen Klopp.

Kikosi hicho cha Anfield bado hakijafanya usajili mpya chini ya kocha mpya Arne Slot. Hivyo Salah anabaki kuwa mchezaji wao muhimu. Je, Liverpool itaongeza mkataba wa Mfalme huyo wa Misri hadi Mei ijayo? Hilo bado halijafahamika.

### Thamani ya Minteh

Moja ya uhamisho wa kustaajabisha wa majira ya kiangazi, ni wa winga wa Gambia, Yankuba Minteh, ambaye msimu uliopita alichezea timu ya Feyenoord ya Uholanzi chini ya kocha Arne Slot.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, alijiunga na Newcastle United akitokea Odense ya Denmark Juni mwaka jana kwa ada ya pauni milioni tano, lakini ghafla akatolewa kwa mkopo.

Baada ya mabao 10 katika mechi 27 za Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, Everton, Lyon na Borussia Dortmund zote zilionesha nia ya kumtaka, lakini Brighton ndiyo iliyolipa pauni milioni 30 kumnunua mchezaji huyo.

Kocha Tom Saintfiet, aliyemchezesha Minteh katika mechi yake ya kwanza ya kimataifa akiwa na umri wa miaka 18, ameimbia BBC Sport Africa kuwa:

"Huu ni msimu wake wa kujifunza kwa kiwango cha juu na kama (Brighton) watamuunga mkono na kumpa muda na kumwacha akue, nina uhakika baadaye katika msimu ataimarika na kuonesha uwezo wake halisi."

### Umuhimu wa Partey Arsenal

Wakati Arsenal ilipotumia pauni milioni 45, kumnunua Thomas Partey Oktoba mwaka 2020, kulikuwa na matumaini angeongeza nguvu na utulivu kwenye safu yao ya kiungo.

Lakini baada ya kucheza mechi 95 za Ligi Kuu England, kwa misimu minne, mchango wa raia huyo wa Ghana umekuwa mdogo kwa sababu ya majeraha ya mara kadhaa.

"Sina hakika kuwa Partey ndiye jina la kwanza kwenye jedwali la timu," anasema mchambuzi wa soka James Cook na mwendesha kipindi cha mtandaoni cha Same Old Arsenal.

"Amepoa sana, hayuko imara kama alivyokuwa huko nyuma. Na hilo linaleta wasiwasi sana."

"Nadhani Arteta alikuwa akitaka kuimarisha safu ya kiungo," anasema Cook, ambaye anaamini klabu hiyo inahitaji kujiimarisha eneo hilo.

### Msimu wa Sarr kung'ara?

Kocha wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou, alipoanza kasi yake msimu uliopita, ilidhihirika kuwa kiungo wa kati wa Senegal, Pape Sarr alikuwa sehemu muhimu ya timu hiyo.

Licha ya jeraha na mapumziko ya katikati ya msimu kwa ajili ya Afcon, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 alianza katika mechi 27 za Ligi Kuu England msimu wa 2023-24.

"Alipoamua kujiunga na Tottenham, wengi walikuwa na shaka kuhusu umbile lake na mahitaji ya Ligi Kuu," anasema Babacar Ndaiye Faye wa BBC Afrika.

"Lakini msimu wake wa kwanza chini ya Postecoglou ulimtuliza kila mtu. Ikiwa Sarr anaweza kujiamini, Spurs watakuwa na mchezaji mzuri."

### Waafrika katika timu zilizopanda

Msimu uliopita ilikuwa ni mara ya pili tangu Ligi Kuu ilipoboreshwa mwaka 1992, ambapo timu zote tatu zilizopanda daraja zilishuka tena.

Ipswich Town, Leicester City na Southampton zitakuwa na matumaini ya kupata mafanikio baada ya Burnley, Luton na Sheffield United zote kufeli.

Leicester wanategemea zaidi wachezaji wa Kiafrika ndani ya kikosi chao, watakuwa na furaha kumpa kiungo mzoefu wa Nigeria, Wilfred Ndidi mkataba mpya.

Nyota wa Zambia, Patson Daka na mshambuliaji wa Ghana, Abdul Fatawu walikuwa washambuliaji wa kikosi cha kwanza msimu uliopita, lakini waliweza kufunga mabao 13 tu kwa jumla katika Ligi ya Championship.

Ipswich imerejea Ligi Kuu baada ya kukosekana kwa miaka 22, chini ya nahodha wao na kiungo wa kati wa Misri, Sam Morsy, na beki wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Axel Tuanzebe, wote watakuwa sehemu ya kikosi hicho.

Vipaji vya Southampton kutoka Afrika vitakuwapo uwanjani, kiungo mshambuliaji kutoka Nigeria, Joe Aribo anatarajiwa kuwamo katika kikosi.

Kocha wa 'Watakatifu' hao, Russell Martin, hivi karibuni alimwita mshambuliaji wa Super Eagles, Paul Onuachu, ambaye alitumia msimu uliopita kwa mkopo huko Trabzonspor, kuwa "mchezaji wa kipee" baada ya maandalizi ya msimu mpya.

Winga wa Ghana, Kamaldeen Sulemana bado hajang'ara katika kipindi cha miezi 18 klabuni hapo na ameondolewa kwenye mechi ya ufunguzi kutokana na jeraha.

## ISIKUPITE

ARSENAL ambayo juzi ilianza msimu kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Wolves, wamependekezwa na wachambuzi 11 kati ya 30 wa BBC TV na redio kuwa mabingwa, huku mshambuliaji wa zamani wa Uingereza Alan Shearer pia akiamini kuwa kikosi hicho cha Mikel Arteta kitashinda - ingawa anafikiri kinaweza kufanya hivyo na mshambuliaji mwingine wa kati na kuipiku Manchester City ambayo inaliwinda taji hilo la Ligi Kuu England kwa mara ya tano mfululizo.



# MAKINDA 11 WA KUTAZAMWA LIGI KUU ENGLAND MSIMU HUU



Kinda wa Arsenal, Ethan Nwaneri, akifanya yake katika mechi ya kirafiki kujiandaa na msimu mpya dhidi ya Manchester United iliyopigwa Marekani mwezi huu. **PICHA: MTANDAO**

**LONDON, England**

SOTE tunawajua nyota maarufu ambao watakuwa katika vichwa vingi vya habari katika msimu mpya - lakini ni wachezaji gani wachanga ambao tunapaswa kuwaangalia?

Waandishi wa soka wa BBC Sport wanachagua baadhi ya vijana wanaotarajiwa kuwa maarufu katika msimu ulioanza Ijumaa iliyopita ya Agosti 16, mwaka huu.

### Trey Nyoni (Liverpool)

Mtangazaji wa BBC Sport, Nizaar Kinsella, anasema: Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 17, amemvutia kocha mpya Arne Slot wakati wa maandalizi ya msimu mpya.

Alifanya vema katika mechi ya kirafiki dhidi ya Real Betis, ambayo ilimfanya apewe sifa na kocha ambaye huwa anasita kufanya hivyo. Nyoni alijiunga na Liverpool kutoka Leicester msimu uliopita wa majira ya joto.

### Josh Acheampong (Chelsea)

Mtangazaji wa BBC Sport, Nizaar Kinsella, anasema: Beki huyo mwenye umri wa miaka 18, alicheza mechi yake ya kwanza na Chelsea msimu uliopita dhidi ya Tottenham Hotspur na alikuwa mmoja wa vijana wawili waliokuwa ziarani nchini Marekani kutoka katika akademi ya timu hiyo. Ni mchezaji bora ambaye anaweza kucheza beki wa kati au kulia.

### Mikey Moore (Tottenham Hotspur)

Mtangazaji wa BBC Sport, Kinsella anasema: Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 16, amekuwa akifunga mabao chini ya kocha Ange Postecoglou katika mechi za kabla ya msimu mpya.

Kinda huyo mwenye kipaji cha hali ya juu alifanya vema katika timu ya vijana chini ya miaka 21 msimu uliopita. Ni mchanga sana kwenda nje kwa mkopo kwa hivyo atabaki na kujichanganya na kikosi cha kwanza.

### Ethan Nwaneri (Arsenal)

Mtangazaji wa BBC Sport, Alex Howell, anasema: Kumekuwa na matarajio mengi kuhusu Nwaneri tangu alipokuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi katika historia ya Ligi Kuu England, alipoanza kuichezea Arsenal akiwa na umri wa miaka 15 katika msimu wa 2022- 23.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17, alicheza mechi moja pekee msimu uliopita kwenye Ligi Kuu dhidi ya West Ham lakini matumaini bado yapo kwa kiungo huyo.

Nwaneri alianza mechi ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya dhidi ya Manchester United nchini Marekani na kutoa pasi ya goli kwa Gabriel Jesus wakati Arsenal wakishinda mechi hiyo.

Iwapo Nwaneri ataendelea kufanya zaidi ya alivyofanya hadi sasa, kuna uwezekano wa kupata dakika nyingi zaidi za kucheza msimu huu.

### Adam Wharton (Crystal Palace)

Mtangazaji wa BBC Sport, Howell anasema: Inashangaza kwamba Adam Wharton alicheza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu Februari mwaka huu.

Uchezaji wake wa kuvutia katika muda mfupi ulimfanya acheze kwa mara ya kwanza England na kujumuishwa kwenye kikosi kilichofika fainali ya Euro 2024.

Vyanzo vya Crystal Palace vinaamini kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ndiye usajili wao bora zaidi kutoka ligi ndogo.

### Jesurun Rak-Sakyi (Crystal Palace)

Howell wa BBC Sport anasema: Rak-Sakyi, alikwenda kwa mkopo Charlton katika msimu wa 2022-23 na alishinda tuzo yao ya mchezaji bora wa mwaka baada ya kufunga mabao 15 na kutoa pasi nne za mabao kwenye Ligi Daraja la Kwanza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, aliumia msimu uliopita na alicheza mechi nane pekee katika mashindano yote akiwa na 'The Eagles' hao. Hata hivyo, amefanya vema katika mechi za kujiandaa na msimu mpya.

### Chido Obi-Martin (Manchester United)

Simon Stone wa BBC Sport anasema: Chido Obi-Martin alicheza kwa miaka miwili iliyopita akiwa Arsenal na anaamini walitoa ofa ya haki kwa mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 16, ambaye amewakilisha England na Denmark katika ngazi ya vijana. Lakini ameamua kujiunga na Manchester United.

Obi-Martin amejidhihirisha kuwa hatari katika safu ya vijana - alifunga mabao 10 katika mchezo mmoja dhidi ya Liverpool chini ya umri wa miaka 16, alipokuwa na umri wa miaka 15.

Itakuwa vema kuona jinsi atakavyoimarika na kama atapata nafasi katika Kombe la EFL na Ligi ya Vijana ya UEFA. Ikiwa atafanya vizuri huko, tunaweza kumuona kwenye benchi la kikosi cha kwanza cha Man United.

### Nico O'Reilly (Manchester City)

Stone wa BBC Sport anasema: O'Reilly mwenye umri wa miaka 19, alifanya vema dhidi ya Barcelona huko Florida. Ingawa baadhi ya nyota wakubwa ndio kwanza wamerejea baada ya michuano ya Euro na Copa America, lakini kiwango cha O'Reilly ni kizuri.

Kiungo huyo wa kati, anajua kucheza mara kwa mara kwenye kikosi cha kwanza haiwezekani kwa sasa kutokana na uwapo wa Rodri. Lakini anaweza kupata nafasi kutokea benchi, haswa baada ya kucheza vizuri katika ushindi wa Ngao ya Jamii dhidi ya Man United.

### Eric da Silva Moreira (Nottingham Forest)

Nottingham Forest ilimleta winga Moreira kutoka St Pauli msimu huu wa majira ya joto kwa chini ya pauni milioni milioni.

Mchezaji wa Kimataifa wa Ujerumani chini ya miaka 17, alicheza mechi yake ya kwanza ya kulipwa msimu uliopita, lakini aliisaidia St Pauli kupanda hadi Bundesliga kwa mara ya kwanza baada ya miaka 13.

Moreira, ambaye anaweza kucheza beki wa kulia, aliisaidia Ujerumani kushinda Ubingwa wa Ulaya chini ya umri wa miaka 17 na Kombe la Dunia mwaka jana.

### Pedro Lima (Wolves)

Wolves walimleta Lima mwenye umri wa miaka 18 kwa pauni milioni 8.5 kutoka Sport Recife Julai, ikiripotiwa kuwa walimpokonya kutoka mikononi mwa Chelsea, na ameonesha kiwango kizuri katika maandalizi ya msimu mpya.

Kadi nyekundu ya Nelson Semedo katika kichapo cha siku ya mwisho kwa Liverpool msimu uliopita, kilimpa Lima fursa ya kujidhihirisha kama beki wa kulia, huku Semedo akifungiwa mechi tatu za mwanzo.

Mchezaji wa Kimataifa wa Ureno, Semedo bado ana uwezo wa kurejea katika nafasi yake, lakini Lima anatarajiwa kuacha alama msimu huu.

### Harrison Armstrong (Everton)

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, amefanya vema katika chuo cha michezo cha Everton na kupata mkataba wake wa kwanza wa kulipwa Julai, na kusaini mkataba wa miaka mitatu.

Kiungo huyo aliingia katika kikosi cha vijana chini ya umri wa miaka 21 msimu uliopita na amepewa nafasi ya kushiriki katika kikosi cha kwanza wakati wa maandalizi ya msimu mpya.

## CHUKUA HIYO...!

ILIMCHUKUA Kai Havertz hadi Novemba 25, mwaka jana, kufunga bao la kwanza akiwa Arsenal - msimu wake wa kwanza, lakini msimu huu imemchukua dakika 25 tu kuzifumania nyavu katika mechi ya kwanza ya msimu mpya.

## Nukuu

Kwa wachezaji wazuri ni hivyo, akiwa na Messi najua atakuja hapa na kuweka mpira pale. Lakini yeye hufanya hivyo kila wakati. Huwezi kumzuia. Huo ndio ubora wa mchezaji. Unapaswa kujua wapi walipo, nini wanataka, kuwapa nafasi na kuwaacha wapumue," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, akielezea kuona kivuli cha Lionel Messi kwa Bukayo Saka akicheza na Kai Havertz kwenye ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Wolves juzi.**



"Hii ndiyo ligi ngumu zaidi duniani na tunajua jinsi ilivyo ngumu kucheza dhidi ya City ila tunajiamini na tunajua ubora wetu na tutaenda kwa hilo," **Winga wa Arsenal, Gabriel Martinelli, kuhusu mbio za ubingwa baada ya kuanza vizuri msimu kwa kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Wolves.**



"Ushindi huo unapendeza sana. Kuanza msimu kwa ushindi siku zote ni muhimu. Hatuko tayari kama kikosi, kama timu, wachezaji wengi hawako fiti kabisa. Tulikuwa na siku 10 tu na timu hii kufanya mazoezi ya pamoja. Natarajia zaidi kutoka kwa timu hii, lakini tuna msingi tunaoweza kujenga juu yake," **Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag, baada ya kufungua msimu wa Ligi Kuu England kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Fulham Ijumaa iliyopita.**




Kocha wa Simba, Fadlu Davids

# LIGI KUU NA MAKOCHA10 WAKIGENI, SITA WAZAWA

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024/25, imeanza Ijumaa iliyopita ikiwa na makocha 10 wakuu wa kigeni huku wazawa wakiwa sita tu ambapo jumla ya timu 16 zitakuwa na safari ndefu ya msimu mzima kusaka ubingwa na zitakazokata tiketi ya kucheza michezo ya kimataifa.

Pamoja na hayo, kama ilivyo safari zote za soka, kuna baadhi ya makocha wanaweza wasifike mwisho wa ligi na wakijikuta wakitimuliwa kutokana na matokeo mabovu au kuondoka wenyewe kwa sababu mbalimbali, hivyo mashabiki watakuwa wakitaka kuona wa kwanza kuondoka atakuwa nani na watakaofikisha majahazi yao mwisho.

Hadi Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita inamalizika, jumla ya makocha 18 walitimuliwa, huku Singida Fountain Gate ikiongoza kwa kutimua wengi zaidi kuliko timu zingine 15 zilizosalia.

Hawa hapo makocha 16 walioanza na timu zao kwenye Ligi Kuu msimu huu, ambao watakuwa wakimulikwa kuona nani ataimaliza safari na atakayefungashiwa virago mapema...

**1# Fadlu Davids - Simba**

Simba itakuwa inanolewa na kocha mpya raia wa Afrika Kusini, Fadlu Davids, ambaye atakuwa si mara ya kwanza tu kuifundisha timu hiyo, bali pia kufundisha Ligi Kuu Tanzania Bara.

Amechukua nafasi ya Abdelhak Benchikha, raia wa Algeria ambaye aliondoka mwenyewe baada ya kuona mambo ni magumu. Kazi yake kubwa ni kuirudisha timu hiyo kwenye heshima yake iliyopotea kwa misimu mitatu, ikipoteza karibuni vikombe vyote iliyokuwa navyo.

**2# Miguel Gamondi - Yanga**

Mpango wake ni kuendeleza alipoishia msimu uliopita au kwenda mbele zaidi kama ikiwezekana. Gamondi raia wa Argentina, anaendelea kuwa Kocha Mkuu wa Yanga kama ilivyokuwa msimu uliopita, ambapo safari hii amesema anataka mataji zaidi, akianza na Ngao ya Jamii, akitaka tena kuwa bingwa wa Ligi Kuu kwa mara ya pili kwake na nne mfululizo kwa Yanga. Ni moja kati ya makocha watano wa msimu uliopita waliobakia kwenye klabu zao msimu huu.

**3# Youssouph Dabo - Azam FC**

Raia huyu wa Senegal ni mmoja kati ya makocha watano wanaoendelea tena kuzifundisha timu za Ligi Kuu msimu huu. Dabo, aliiwezesha Azam FC kumaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, hivyo mabosi kuendelea kumwamini kwa kumpa jukumu la

2015, na msimu uliopita kwa nyakati fulani alikuwa Kocha Mkuu wa Tabora United.

Msimu huu amekabidhiwa jukumu la kuifundisha timu iliyopanda Ligi Kuu, Pamba Jiji. Malengo aliyopewa ni kuibakisha Ligi Kuu.

**5# Patrick Aussems - Singida Black Stars**

Ligi Kuu ina kocha raia wa Ubelgiji, Patrick Aussems, akiifundisha timu ya Singida Black Stars. Huyu pia ni mgeni kwenye ligi, kwani amewahi kuifundisha Simba 2018 hadi 2019.

Safari hii anaifundisha Singida, akiwa mmoja kati ya makocha wapya walioingia msimu huu, lengo ni kuifanya timu hiyo kufuzu kucheza mechi za kimataifa mwakani.

**6# Paul Nkata - Kagera Sugar**

Mmoja kati ya makocha wanaofundisha kwa mara ya kwanza soka la Tanzania ni Paul Nkata, raia wa Uganda.

Amechukuliwa kukinoa kikosi cha Kagera Sugar, ambacho msimu uliopita kilinusurika katika mwishoni kucheza mechi za mchujo au kushuka daraja. Amechukuliwa kwa lengo moja tu, kuhakikisha inabaki salama Ligi Kuu bila presha ya michezo ya mwisho.

**7# Abdihamid Moalin - KMC**

Ni kocha mzoefu kwa sasa katika Ligi Kuu ya Tanzania, akiwa na misimu mitatu. Awali aliifundisha Azam FC, na msimu uliopita alikinoa kikosi cha KMC, ambacho kilimaliza nafasi ya tano. Moalin mwenye uraia pacha wa Somalia na Marekani, msimu huu ameaminiwa tena na Manispaa ya Kinondoni kuendelea kukinoa kikosi hicho.

**8# David Ouma - Coastal Union**

Ligi ya Tanzania ina kocha mwingine raia wa kigeni, huku akitoka Kenya, akikinoa kikosi cha Coastal Union.

Alianza kukifundisha kikosi hicho katikati ya kipindi cha dirisha dogo la usajili na kuitoa chini mpaka kuiwezesha kushinda nafasi ya nne, kiasi cha kupata tiketi ya kucheza mechi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika. Muite David Ouma.

**9# Mwinyi Zahera - Namungo**

Pamoja na kwamba ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, lakini Mwinyi Zahera ni mmoja wa makocha wazoefu katika Ligi Kuu Tanzania Bara tangu 2021, alipoanza kuinoa Yanga hadi 2023.

Baadaye alikwenda Polisi Tanzania, na Coastal Union na sasa ndiye Kocha Mkuu wa Namungo, akiingia msimu wa pili sasa.

**10# Francis Kimanzi - Tabora United**

Nchi ya Kenya, ndiyo inaongoza kuwa na makocha wengi wa kigeni kwenye Ligi Kuu ya Tanzania, kwani baada ya Ouma wa Coastal Union, kuna Francis Kimanzi, kocha mpya kabisa ambaye amekuja kuifundisha Tabora Union msimu huu.

**11# Mbwana Makata - Prisons**

Makocha sita wa Kitanzania ambao wameanza mwanzo wa msimu na timu zao, wanaongozwa na Mbwana Makata, ambaye anakinoa kikosi cha Prisons. Si mgeni kwenye Ligi Kuu, lakini msimu uliopita alikuwa akikinoa kikosi cha Pamba Jiji na ndiye aliyekipandisha daraja.

**12# Mecky Maxime - Dodoma Jiji**

Kocha mzawa, Mecky Maxime, anakiongoza kikosi cha Dodoma Jiji kwenye kinyang'anyiro cha kuusaka ubingwa wa Tanzania Bara. Atakuwa anakinoa kikosi hicho kwa mara ya kwanza, lakini akiwa mzoefu kwenye Ligi Kuu, kwani amezifundisha timu nyingi, zikiwamo Kagera Sugar, Mtibwa Sugar na Ihefu.

**13# Mohamed Abdallah - Mashujaa FC**

Kwa msimu wa pili mfululizo, Bares atakiongoza kikosi cha Mashujaa FC kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Na hii ni baada ya viongozi kuridhishwa na uwezo wake, licha ya kwanza ilisubiri mechi ya mwisho dhidi ya Dodoma Jiji msimu uliopita ili kubaki Ligi Kuu.

**14# Mohamed Muya - Fountain Gate**

Fountain Gate inanolewa na mmoja wa makocha bora nchini, ingawa hana jina kubwa sana, Mohamed Muya.

Timu hiyo ambayo msimu uliopita ilijulikana kama Singida Fountain Gate, imempa malengo kocha huyo ya kuibakisha Ligi Kuu.

**15# Fikiri Elias - KenGold**

Fikiri Elias yeye amebeba jukumu la kuinoa timu inayocheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu huu, KeGold. Ikumbukwe kabla ya kuwa kocha wa timu hiyo, ameshawahi kuwa kocha msaidizi wa Coastal Union na kuna wakati alikuwa akikaimu kama kocha mkuu.

**16# Ahmad Ally - JKT Tanzania**

Baada ya kuiwezesha Prisons kufanya vema kwenye Ligi Kuu msimu uliopita, msimu huu atakuwa na kazi ya ziada kuhakikisha pia JKT Tanzania inafanya vizuri.

Ahmad Ally, amechukua nafasi ya Malale Hamsini, huku yeye mwenyewe nafasi yake Prisons, ikichukuliwa na Makata.

## JE, WAJUA?



BAO alilofunga Mohamed Salah juzi wakati Liverpool ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ipswich Town, limemwezesha kuweka rekodi ya kuwa kinara wa mabao ya mechi za wiki ya kwanza za ufunguzi za msimu mpya wa Ligi Kuu England baada ya kufikisha mabao tisa mbele ya Frank Lampard, Wayne Rooney na Alan Shearer waliofanya hivyo mara nane tu.





# Wanawake vyama vya siasa kupewa mafunzo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WANAWAKE zaidi ya 250 nchini wanatarajiwa kupatiwa mafunzo ya uraia na kujengewa uwezo, ili waweze kugombea katika nafasi mbalimbali za uamuzi ikiwamo Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu, kupitia mradi wa mabinti uchaguzini.

Mradi huo unafadhiliwa na Shirika la IRI na kushirikiana na shirika linalojihusisha na utoaji wa elimu ya uraia kwa wanawake vijana nchini la Her Uraia Clickers.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Nyangubu Nyamsogoro, alibainisha hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafunzo kwa wanawake vijana kutoka vyama vya siasa vitatu mkoani Dodoma.

Nyamsogoro alisema mafunzo hayo yametolewa kwa vijana kutoka vyama vya siasa vitatu ambavyo ni Chama cha Mapinduzi (CCM), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) pamoja na ACT-Wazalendo.

Aidha, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wanawake vijana kugombea katika nafasi mbalimbali za maamuzi badala ya kuendelea kuwa watu wa kuwatafutia kura wengine.

Alisema hivi sasa takwimu zinaonyesha kuwa katika daftari la wapigakura wanawake ni wengi kuliko wanaume lakini kwenye kugombea wamekuwa wachache.

"Mafunzo haya leo ni mwendelezo wa yale ambayo tumeyatoa mkoani Pwani lakini lengo letu ni kuwajengea uelewa wanawake vijana ili waweze kuthubutu kugombea katika nafasi mbalimbali za maamuzi," alisema.

Kadhalika, alisema wamepanga kutoa mafunzo hayo kwa mabinti wenye umri mdogo ambao wapo kwenye vyama vya siasa ili kuondoa mtazamo ulipo hivi sasa wa wanawake kutumika kupiga kura na siyo kugombea.

Ofisa Miradi wa shirika hilo, Josephat Raphael, alisema mafunzo hayo ni ya awamu ya pili baada ya yale yaliyofanyika mkoani Pwani ambapo lengo ni kuwafikia wanawake vijana zaidi ya 200.

Alisema pamoja na kutoa mafunzo hayo pia wamekuwa wakitumia matamasha na mkongamano mbalimbali nchini kuwafikia wanawake vijana na kuwajengea uwezo kushiriki kugombea katika nafasi za maamuzi.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Sabitina Makweta, alisema yatakuwa chachu kwa wanawake vijana nchini kujitokea kugombea katika nafasi za maamuzi ikiwemo Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu.



Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Her Uraia Clickers, Nyangubu Nyamsogoro, akitoa mafunzo juzi jijini Dodoma ya uraia na masuala ya uchaguzi kwa wanawake vijana kutoka vyama vya siasa mkoani humo, kupitia mradi wa mabinti uchaguzini. **PICHA: PAUL MABEJA**

## DC aagiza watumishi afya kutekeleza afua za lishe

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali, amewataka watumishi wa afya pamoja na watendaji wa kata na vijiji kufanya kazi kwa bidii, ili kufikia malengo yaliyowekwa na serikali ya utekelezaji wa afua za lishe wilayani hapa.

Alisema hayo juzi wakati wa kikao cha tathmini ya lishe, jiongeze tuwavushe salama na bima ya afya iliyoboreshwa cha robo ya nne kwa mwaka wa fedha 2023/24, kilichofanyika katika ukumbi wa mkutano wa Mkuu wa Wilaya ya Mkalama.

"Kila mtu atimize wajibu wake, tufanye kazi kwa bidii tuweze kufikia malengo yaliyowekwa, wakuu wa vituo vya kutolea huduma za afya na watendaji hakikisheni mnasimamia watumishi wenu, hatutavumilia watu wanaotufelisha," alisema.

Machali alisema watumishi wote walioshindwa kufikia malengo yaliyowekwa watawajibishwa kwa mujibu wa taratibu na sheria za kiutumishi zilizopo.

Akizungumzia suala la bima za afya, alitoa wito kwa watendaji kutumia vyema mikutano ya vijiji kutoa elimu juu ya umuhimu wa kukata Bima ya Afya ya iCHF iliyoboreshwa pamoja na NHIF.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Selemani Msunga aliwataka watendaji kuhakikisha wanatekeleza suala la lishe katika shule zote zilizopo wilayani Mkalama.

Akiwasilisha taarifa juu ya hali ya utekelezaji wa afua za lishe wilayani Mkalama, Kaimu Ofisa Lishe Wilaya, Ernest Makori alisema asilimia 75.37 ya wanafunzi wilayani humo wanapata chakula shuleni.

**Machali alisema watumishi wote walioshindwa kufikia malengo yaliyowekwa watawajibishwa kwa mujibu wa taratibu na sheria za kiutumishi zilizopo.**

## RC atoa siku 10 watendaji kukamilisha miradi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amewaagiza watendaji katika halmashauri kuhakikisha wanakamilisha utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo ifikapo mwishoni mwa mwezi huu.

Alitoa agizo hilo jana katika majumuisho ya ziara yake ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo katika Manispaa ya Singida.

Dendego alisema kuwa miradi yote iliyoanza kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu nyuma lazima ikamilike, ili wananchi waanze kupata huduma mbalimbali za kijamii kwa muda muafaka.

"Lengo la miradi hii siyo kuona majengo bali ni kutoa huduma inayotakiwa lazima majengo yakamilike kwa wakati na kwenye matatizo viongozi wakae na kutatua changamoto hiyo ili miradi isikwame," alisema.

Alisema maeneo yote ya miradi ambayo yana migogoro lazima viongozi wakae wahusika ili kuondoa changamoto hizo kwa wakati nia ikiwa ni kuona wananchi wanaanza kupata huduma bora na za msingi karibu na maeneo yao.

Dendego pia alipongeza hatua zinachukuliwa na watendaji katika kusimamia na kutekeleza miradi hiyo ya maendeleo ili iweze kutekelezwa kwa viwango na ubora unaotakiwa.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, alimhakikishia Mkuu wa Mkoa wa Singida kuwa atahakikisha miradi yote inayotekelezwa mkoani humo inakamilika kwa wakati na kwa kuzingatia thamani ya fedha iliyotolewa.

Dk.Mganga aliwasisitiza watendaji wote washiriki kikamilifu katika kusimamia miradi iliyopo kwenye maeneo yao, ili wananchi waweze kufurahia huduma bora zinazotolewa na serikali.

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe, alisema atafanya kazi kwa usiku na mchana na kwa ushirikiano na watendaji wengine ili kuhakikisha miradi yote ya maendeleo inayotekelezwa wilayani mwake inakamilika ifikapo mwisho wa mwezi huu.

## WCF yatoa msaada vyerehani 30 kituo kulea watoto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi nchini (WCF) umetoa msaada wa vyerehani 30 kwa kituo cha makao ya taifa ya kulea watoto Kikombo jijini Dodoma.

Mkurugenzi Mkuu wa WCF, John Mduma, akikabidhi msaada huo juzi kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, alisema vyerehani hivyo vitasaidia kutoa mafunzo kwa watoto wanaolelewa kituoni hapo.

"Msaada huu ni moja kati ya utelezaji wa sera yetu ya kurudisha kwa jamii, utakwenda kusaidia kituo hicho cha makao ya taifa ya kelea watoto kutoa mafunzo lakini pia kuongeza kipato," alisema.

Ridhiwan aliupongeza uongozi wa WCF, kwa kutoa msaada huo ambao alisema utakwenda kusaidia watoto hao kujifunza ushonaji.

Alisema: "Watoto hawa wote siyo watakuwa waandishi wa habari au walimu wengine watakuwa mafundi, hivyo msaada huu utakwenda kusaidia kuwaongezea ujuzi lakini pia kuongeza mapato kwa kituo kwa watu ambao watakuja kujifunza hapa mambo ya ushonaji".

Alisema ameridhishwa na mazingira ya kituo hicho ambayo kinaendesha shughuli za kuhudumia watoto kutoka maeneo mengi ya nchi.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu, Zuhura Yunusi, aliupongeza mfuko wa WCF, kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali za kuweka mazingira rafiki ya malezi kwa watoto.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ally Hamis, alisema watoto katika kituo hicho wanalelewa kwa kuzingatia maadili na utamaduni wa kitanzania.





# DC anusa ufisadi mradi wa vyoo, maji zahanati za vijiji vinne

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

MKUU wa Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe, Victoria Mwanziva, amenusa harufu ya ubadhirifu kwenye mradi ya uboreshaji miundombinu ya maji na vyoo katika zahanati za vijiji vinne wilayani humo.

Mwanziva aliyasema hayo wakati akiwasilisha salamu za serikali kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa cha robo ya nne ya mwaka 2023/2024, kilichofanyika katika ukumbi wa halmashauri hiyo.

Hivyo, aliagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilayani humo kuchunguza miradi hiyo na kwamba watakaobainika kuhusika na ubadhirifu wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Alisema hivi karibuni alifanya ziara ya kushtukiza ya kukagua utekelezaji wa mradi wa uboreshaji miundombinu ya maji na vyoo katika zahanati za vijiji vinne vya Luilo, Mbwila, Mawengi na Manga ambazo kila moja ilipatiwa Sh. milioni 40.

Alifafanua kwamba kwenye ukaguzi huo alibaini kufanyika uhuni kwenye manunuzi ya vifaa ambapo watumishi walikuwa wanaoogeza bei tofauti na uhalisia wa bei.

Alisema mfuko mmoja wa saruji ambao Ludewa hununuliwa kwa Sh. 18,000 hadi Sh. 20,000 umenunuliwa kwa Sh. 30,000, tangi la maji la lita 5,000 ambalo linauzwa Sh. 900,000 limenunuliwa kwa Sh. milioni 1.5, fremu moja ya mlango wa kawaida umenunuliwa kwa Sh. 365,000 badala ya Sh. 150,000.

Vilevile alisema vipo vifaa vingine vidogo vidogo yakiwamo makufuli, masinki ya vyoo ambavyo pia vimenunuliwa kifisadi hali ambayo alidai hawezi kuvumilia.

“Nilipoanza tu ziara nikajua kuwa kuna Sh.milioni 78 kwa ajili ya usimamizi wa ujenzi wa uboreshaji miundombinu ya maji na vyoo ambazo nilizitilia mashaka nikaitisha nyaraka na nikabaini kuwa zimesalia Sh. milioni 21 pekee,” alisema Mwanziva.

Hivyo, aliwatahadharisha watumishi wa halmashauri hiyo kuepuka kutumia vibaya fedha za serikali, akisisitiza kuwa watachukuliwa hatua kali za kiutumishi na za kijinai ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia za aina hiyo.

Alisema atahakikisha anasimamia miradi yote ya maendeleo wilayani humo na kuhakikisha inatekelezwa kwa viwango vinavyotakiwa kwa mujibu wa miongozo ya serikali.

Hata hivyo, alisema imezoeleka kuwa watumishi wanapofanya uharibifu wa kazi ikiwemo ubadhirifu wanaamishwa kituo cha kazi jambo ambalo hataki kuliona likitokea na badala yake afukuzwe kabisa kazi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Wise Mgina, alimshukuru Mkuu wa Wilaya kwa kufanya ziara ya kushtukiza kwa maelezo kuwa imewasaidia kuibua baadhi ya mambo ambayo yalikuwa hayaendi sawa.

Alisema hata wao kama madiwani walifanya ziara kwenye baadhi ya miradi na kwamba walipohitaji baadhi ya nyaraka muhimu za miradi waliambiwa kuwa zilishachukuliwa na mkuu huyo.



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (katikati), akimsikiliza mmiliki wa mgodi wa madini ya Green Garnet, Joseph Mwakipesile maarufu Chusa (wa pili kushoto), akielezea changamoto za maji, umeme na barabara alipotembelea machimbo ya Lemshuku juzi, kulia ni Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka na kushoto ni Ofisa Madini Simanjiro, Nchagwa Marwa. **PICHA: GIFT THADEY**

# W’biashara Soko la Igawilo wagoma kulipa ushuru

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAFANYABIASHARA wa Soko la Igawilo jijini Mbeya wamegoma kutoa ushuru wakipinga utaratibu ulioanzishwa na Jiji hilo wa kuwatoza Sh. 9,000 kwa mwezi, badala ya Sh. 300 ambayo wamekuwa wakitozwa kila siku.

Pia, wanadai kuwa halmashauri imewapora choo ambacho walikijenga kwa nguvu zao, ikitaka ianze kukiendesha yenyewe huku wakieleza kuwa hawajawahi kushirikishwa chochote.

Walitangaza msimamo huo wakati wa mkutano wa hadhara ulioitishwa na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na kufanyika katika soko hilo na kuhudhuriwa na baadhi ya watendaji wa jiji hilo.

Ephrahim Ngusa alisema utaratibu wa awali wa ukusanyaji wa Jiji ulikuwa hauna shida yoyote kwa maelezo kuwa kila mfanyabiashara alikuwa anatembelewa kwenye eneo lake na kutoa Sh. 300.

Alisema utaratibu mpya wa kusubiri mpaka mwisho wa mwezi ndiyo halmashauri ikakusanye Sh. 9,000 unawasababishia wafanyabiashara hao kuwa na mzigo mkubwa kutokana na kwamba mitaji yao ni midogo.

Naye Amina Lule alisema wao kama hawatarudishiwa utaratibu wa awali wataendelea kutokutoa ushuru mpaka halmashauri itakapobadili msimamo wake.

Alisema choo cha soko hilo wakilijenga wenyewe kwa kuchangishana na waliweka utaratibu wa namna ya kukiendesha, lakini kwa sasa halmashauri inataka kuwapora ili wakiendesha.

Alisema walikuwa wanaajiri mtu ambaye alikuwa anakisimamia kwa makubaliano maalumu na kumlipa kila mwezi na hakijawahi kuleta shida, hivyo wanashangaa hivi sasa kwanini waporwe.

Ofisa Masoko wa Jiji la Mbeya, Furaha Mkonongo, alisema soko hilo lina wafanyabiashara zaidi ya 400, wengi wao ni wa maduka na wajasiriamali wadogo na kwamba halmashauri imeajiri watu wawili ambao wamekuwa wakikusanya ushuru kila siku.

Vilevile alisema halmashauri iliamua kubadili mfumo wa usimamizi wa choo ili kuongeza ufanisi na kuongeza mapato pamoja na kukiboresha choo hicho.

Hata hivyo kutokana na wafanyabiashara kutokubaliana na mfumo huo, Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, John Nchimbi aliridhia kurejeshwa kwa utaratibu wa awali wa ukusanyaji wa ushuru wa Sh. 300 kila siku kama ambavyo wafanyabiashara walikuwa wanataka.

Alisema pamoja na kurejesha utaratibu huo lakini watawagawa wafanyabiashara hao katika makundi ya watu 20 kila moja na kila kundi litakuwa na kiongozi ambaye atakuwa anakusanya ushuru kwa niaba ya serikali na kuwasilisha halmashauri.

“Tutaweka utaratibu kama wa nyumba 10, na hapa kwa sababu mpo 400 tutatengeneza makundi 20 lakini hili la choo tunawarejeshea lakini mtakuwa mnatupatia taarifa na sisi tutakuwa tunawapatia taarifa kila mwezi,” alisema Nchimbi.

Akizungumza na wananchi hao, Dk. Tulia aliwataka kuwa waaminifu katika ulipaji wa ushuru kwa madai kuwa ushuru huo ndio unatumika kuboresha huduma mbalimbali katika maeneo yao ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa.

# Wanafunzi Tarafa ya Kipembawe watangaziwa neema

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMPUNI ya ununuzi wa tumbaku ya premium imetangaza kuwasomesha wanafunzi wawili kutoka Tarafa ya Kipembawe wilayani Chunya, watakaofaulu mtihani wa kidato cha nne kwa kupata daraja la kwanza.

Ofisa TEHAMA wa kampuni hiyo, Delister Hyera alitoa ahadi hiyo mwishoni mwa wiki aliposhiriki ziara iliyoandaliwa na Ofisa Tarafa wa Tarafa ya Kipembawe, Kassim Kirondomara ya kuwahamasisha wanafunzi kusoma kwa bidii.

Alisema kila shule atachaguliwa mwanafunzi mmoja wa kike na wa kiume ambao watasomeshwa na kampuni hiyo kwa kulipiwa gharama zote katika shule watakazopangiwa.

Alisema kampuni hio imeamua kuwasomesha wanafunzi hao ikiwa ni sehemu ya urejeshaji wa sehemu ya faida kwa jamii pamoja na kuanzisha utaratibu wa kuwekeza kwa vijana.

“Hii ni ahadi ya kampuni, sasa na mimi nitakuwa na zawadi yangu binafsi kwa mdada atakayefanya vizuri, nitamshonea sare za shule (uniform) kokote anatakokwenda kusoma masomo yake ya ‘A level’ niwaombe mpambane ili mnufaike na ahadi hizi,” alisema Delister.

Awali Ofisa Tarafa wa Tarafa ya Kipembawe, Kirondomara alisema kwa tarafa hiyo ina kata tisa ambazo kwa sasa zimebaki kata mbili pekee ambazo hazina shule za sekondari ambazo ni Upendo na Nkung’ungu.

Alisema Kata ya Upendo wananchi wameanza kujenga shule kwa nguvu zao na Kata ya Nkung’ungu serikali imeshatoa Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa shule.

Alisema kati ya kata zote zenye shule za sekondari ni nne pekee ambazo zimefika kidato cha nne ambazo ni Isangaana, Mtanila, Mtande na Lupa ambayo imefika mpaka kidato cha sita.

Alisema mbali na kuhamasisha wanafunzi kusoma kwa bidii, pia ziara hiyo ilikuwa na lengo la kuwahamasisha wanafunzi kuepuka vitendo viovu ikiwamo kushiriki mapenzi katika umri mdogo na matumizi ya dawa za kulevya.

Tarafa ya Kipembawe ndiyo inayoongoza kwa uzalishaji wa tumbaku katika Wilaya ya Chunya na ndiyo inayoifanya wilaya hiyo kuwa Mkoa wa Kitumbaku.





## Rais Dk. Mwinyi kuongoza mapokezi ndege mpya leo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NGEGE mpya aina ya Boeing B787-8 Dreamliner inayomilikiwa na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), inatarajiwa kuzinduliwa leo Zanzibar na Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Ngege hiyo yenye uwezo wa kubeba abiria 262 ambapo viti 22 ni vya daraja la biashara na viti 240 ni daraja la kawaida pia ina uwezo wa kubeba mizigo kati ya tani 15 hadi 20.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzinduzi wa ndege hiyo, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa, alisema kupokelewa kwa ndege hiyo ya masafa marefu kunaiwezesha ATCL kuwa na ndege 16.

Alisema kati ya ndege hizo 15 ni mpya, zimenunuliwa kutokana na mpango wa ufufuaji wa ATCL ulioanza kutekelezwa mwaka 2016.

"Kununuliwa kwa ndege hii ya Dash 8-Q400 kutafanya serikali iwe imenunua ndege nane mpaka hivi sasa. Ndege hiyo itakapowasili Serikali itakuwa na ndege mpya 16 zilizonunuliwa kutokana na mpango wa mkakati wa kuifufua Shirika la Ndege ya Tanzania (ATCL) ulioanza mwaka 2016, " alisema.

Alisema serikali imeendelea kuhakikisha kuwa ATCL inatoa huduma zenye kuhimili ushindani katika soko la kikanda na kimataifa kwa kuanzisha safari za moja kwa moja.

Profesa Makame alisema kwa sasa, ATCL inahudumia vituo vya ndani 14 ambavyo ni Mwanza, Bukoba, Songea, Zanzibar, Katavi, Dar es Salaam, Geita, Kigoma, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, na Tabora.

Alisema ATCL inahudumia vituo vya kikanda na kimataifa ambavyo ni Entebbe- Uganda, Nairobi, Burundi, Comoro, Lubumbashi, DRC, Lusaka, Zambia, Zimbabwe, India, Guangzhoa – China na Dubai - UAE.

Hata hivyo alisema ujio wa ndege hiyo kutaiwezesha ATCL kuongeza safari zake kwa vituo vya kikanda na kimataifa ambavyo wanahudumia kwa sasa pamoja na kuanzisha safari mpya za Kinshasa, Goma, Muscat na Lagos.

Alisema serikali inaendelea kuwa na usimamizi wa karibu kwa ndege zote, mitambo na vifaa vilivyonunuliwa kwa kuhakikisha kuwa zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa kulingana na mpango biashara wa ATCL.

Akizungumzia kuhusu kukamatwa kwa ndege za ATCL kutokana na madeni, Kaimu mkurugenzi wa ATCL, John Nzunda, alisema serikali imeshalipa madeni mengi ambayo yalikuwa yanachangia tatizo hilo.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum alisema suala la usafiri wa anga ni muhimu katika kukuza uchumi wa nchi na kuleta ustawi mzuri kwa wananchi.

Alisema serikali zote mbili zinaendelea kufanya kazi kubwa ya kuimarisha miundombinu ya usafiri wa anga na kuleta ndege kubwa.

Dk. Khalid alisema uzinduzi wa ndege hiyo Zanzibar itasaidia kuiunganisha na nchi za ndani na mataifa mengine na kukuza uchumi kupitia stekta ya utalii.

# Zanzibar kuwa kitovu cha matibabu Afrika Mashariki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, amesema muda mfupi ujao mapinduzi makubwa ya afya yatafanyika visiwani Zanzibar.

Amesema mapinduzi hayo yataiwezesha Zanzibar kuwa kitovu cha matibabu ya watalii Afrika Mashariki.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya utiaji saini makubaliano ya usajili wa matibabu ya afya kwa njia ya kidijitali kati ya wizara yake na Kampuni ya Tancloud pamoja na Kampuni ya Electronics Health Network ya Uingereza.

Alisema afya ni mtaji na ndiyo maana serikali inatumia fedha nyingi kwa ajili ya kugharamia, hivyo serikali itahakikisha inalinda afya za wananchi wote.

"Tunataka ulimwengu mzima utambue kuwa Zanzibar ni kitovu cha mtaji wa afya, naamini kwamba katika kipindi kifupi kijacho kutatokea mabadiliko makubwa sana ya huduma za afya," alisema.

Alisema TEHAMA itaikomboa Zanzibar katika kutoa huduma nzuri ya afya na kila mtu atapata huduma ya uhakika kwa muda mfupi na kuridhika na huduma anayoipata.

Mazrui alisema serikali inataka kuona kuwa huduma ya afya inayotolewa Zanzibar haina tofauti na nchini India, Afrika Kusini au Ulaya.

Alisema hakuna haja ya Wazanzibari kwenda kutafuta matibabu nje ya nchi wakati huduma hizo zinapatikana nchini.

Hata hivyo, alisema serikali haijabinafsisha huduma za afya katika hospitali zake za wilaya, mkoa na rufaa bali inashirikiana na sekta binafsi katika uendeshaji wa huduma hospitalini humo.

Pia alisema serikali inashirikiana na sekta binafsi ili kuongeza ufanisi na wananchi wapate huduma za afya safi na salama. Alisema wamebaini kuwa wananchi wengi wanapenda kwenda kutibiwa katika hospitali binafsi na wanatumia fedha nyingi na wale ambao hawana uwezo hutafuta wafadhili ili wasaidiwe matibabu.

Aidha, alisema wametiliana saini ya makubaliano hayo ili kushirikiana na kuleta teknolojia za kisasa katika hospitali na vituo vya afya na mfumo wa uingizaji na usambazaji wa dawa.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Tancloud, Sumeya Okod, alisema makubaliano hayo ni ya miaka sita, yatagharimu zaidi ya Dola za Marekani milioni 170.

Alisema katika kitu watakachokiangalia katika utoaji wa huduma za afya ni matumizi ya teknolojia ya kisasa kwa njia ya kidijitali ili Zanzibar ipige hatua katika utoaji wa huduma za afya.




Makamu Mwenyekiti wa Taifa wa ACT-Wazalendo Tanzania Bara, Is-Haka Mchinjita, akizungumza na wananchi wa Jiji la Tanga katika mkutano wa hadhara uliofanyika eneo la Mabanda ya Papa wakati wa ziara yake mkoani humo juzi, yenye lengo la kuhamasisha wanachama kujitokeza kwa wingi kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka huu. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

# UVCCM yaunga mkono matumizi nishati safi

**Na Gwamaka Alipipi**

MWENYEKITI wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Mohammed Ally Kawaida, amesema UVCCM imedhamiria kuunga mkono matumizi ya nishati safi ya gesi kwani yana umuhimu katika kuimarisha maisha ya vijana na maendeleo ya taifa.

Alisema hayo jana Zanzibar wakati akishirikiana na viongozi wenzake wa UVCCM kukabidhi mitungi ya gesi 200 kwa wajumbe wa baraza la umoja huo Unguja.

Alisema kupitia teknolojia hiyo, vijana wanauwezo mkubwa kwa kujenga misingi ya mazingira safi, afya bora, na maendeleo endelevu.

"UVCCM, kama jumuiya yenye dhamana ya vijana wa kitanzania, inaendelea kutimiza wajibu wake katika kuhakikisha vijana wanakuwa sehemu ya mabadiliko haya kwa maendeleo ya taifa," alisema.

Alisema UVCCM wanatambua kuwa mustakabali wa taifa upo mikononi mwa vijana, hivyo wanatekeleza wajibu wao wa kuwawezesha vijana ili wawe sehemu ya kuchangia maendeleo ya taifa.

Kawaida alisema kugawa mitungi ya gesi ni hatua muhimu katika kuwapa vijana nishati safi, ambayo itawasaidia katika shughuli zao za kila siku na kuboresha maisha yao.

Kadhalika, aliwasisitiza viongozi kudumisha umoja na mshikamano kwa maslahi mapana ya CCM na maendeleo ya taifa.

Alisema jukumu la UVCCM ni kuhakikisha vijana wa Kitanzania wanapata nyenzo muhimu zinazowawezesha kuwa viongozi bora na raia wa mfano, ili kujenga Tanzania yenye maendeleo.

## Uoto wa miti ya matunda, misitu ya asili wapotea Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amesema uoto wa miti ya matunda na misitu ya asili Zanzibar unaendelea kupotea kutokana na jamii kuacha utamaduni wa urithi wa wazee wa kupanda na kutunza miti.

Alisema hayo Nyamanzi Wilaya ya Magharib B Unguja, wakati wa uzinduzi wa proramu ya kitaifa ya kurithisha Zanzibar ya kijani kwa wananchi.

Pia ililenga kurejesha utamaduni wa kupanda na kutunza miti ikiwamo ya matunda, uoteshaji na uhifadhi wa misitu, miti ya kivuli pamoja na mbao.

Alisema serikali ilianzisha jitihada za kuifanya Zanzibar kuwa ya kijani tangu mwaka 1964 ikiwamo upandaji wa miti ya mipira, minazi sambamba na uhamasishaji wa wananchi kuendelea na kilimo cha viungo.

Pia, kutunga sera na sheria mbalimbali ili kusaidia kulinda na kuhifadhi ukijani wa Zanzibar.

Hata hivyo, alisema pamoja na jitihada hizo kuendelea, uoto na ukijani wa asili Zanzibar unaendelea kupotea kutokana na jamii kuwa na tabia ya kukata miti waliyoikuta ambayo wazee walipanda.

Othman alisema kutokana hali hiyo, serikali imekuja na mpango huo wa kitaifa ili kurejesha utamaduni kwa jamii kupenda kupanda na kuitunza miti ambao utakuwa shirikishi kwa taasisi, majeshi, wanafunzi na vikosi mbalimbali pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali.

Aidha, alisema kwamba juhudi hizo pia zinakusudia kuwaleta pamoja wadau kutoka sekta na ngazi tofauti baada ya kuona kwamba yapo mambo mengi yanayosababisha upoteaji mkubwa wa miti na misitu.

Hivyo, aliwataka wananchi, wafanyabiashara, wawekezaji , vikosi vya ulinzi na usalama, wanafunzi kuhakikisha wanashiriki katika utekelezaji wa mpango huo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman, alisema mpango huo ni muhimu kwa vile kijani ya Zanzibar imepotea, licha kwamba ni muhimu kwa kizazi cha sasa na baadaye.

Alisema kutokana na hali ya ukame baadhi ya mataifa mengi duniani yamekuwa yakipata shida kutokana na ongezeko la joto kulikosababishwa na kukosekana kwa miti kwenye nchi hizo.

Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Iliyasi Pakacha Haji, alisema mpango huo utaibadili Wazanzibar kuwa na mitazamo kwamba miti na misitu inapaswa kutunzwa, kuirithisha jamii ya sasa na ya baadaye.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASSPORT YA KUSAFIRIA



**MOTA CECILIA MLAMA** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye namba **TAE 314307** iliyotolewa na makao makuu DAR ES SALAAM mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/172600/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**APPOLENIA AGATHER MBOWE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV4** yenye usajili namba: **T 837 DSS,** CHASSIS NAMBA: **ACA365007044** na ENGINE NAMBA: **2AZEAA303938.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/172942/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FANZURI SAIDI MSUYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **SUZUKI KERRY** yenye usajili namba: **T 344 DHR,** CHASSIS NAMBA: **DB52T111427** na ENGINE NAMBA:**F6AEAA1427.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/147612/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YUDA EDMUND SOKA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **KLUGER** yenye usajili namba **T 569 DGS,** CHASSIS NAMBA: **ACU250018452** na ENGINE NAMBA : **2AZ0887705.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/171820/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HASSANI MUSTAFA HASANI** anatangaza kupotea kwa kadi za gari aina ya **TOYOTA HIACE** zenye usajili namba: **T 745 AJA,T 699 AHH, T 852 ABD.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **KGR/TR/RB/523/2024 KGR/TR/RB/522/2024 KGR/TR/RB/521/2024**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT DELEGATED COURT OF MOROGORO**
**AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.17692 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JOSEPH AUGUST NGALLO-THE DECEASED**

**AND IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY MARY JOSEPH MATILYA**

**MARY JOSEPH MATILYA....................................PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Made under rule 75 of the probate and administration of Estate rule, CAP 352 R,E 2019)**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above-named pepetitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 20th day of 08,2024.

DATED and SIGNED at Morogoro this 24th day of JULY,2024.

Senior resident magistrate
Morogoro District Court

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**

**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 18102 of 2024**

**In the matter of the Estate of the Late JOHN MWINAMO LYAYUKA.**

**And**

**In the Matter of Application for letters of administration by**
**LAWRENCE JOHN LYAYUKA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above -named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 19th day of AUG.2024

Daled at DAR ES SALAAM this 30th day of JULY 2024.

Principal Resident Magistrate

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya SINGIDA**
**Kituo cha UTEMINI, Mkoa SINGIDA**

**Shauri la madai Na 146/2024**

**Jina la mdai..........................................ESTHER SHELUKINDO**

**Jina la mdaiwa......................RAINFRIDA ALEXANDER REMMY**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**( kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa RAINFRIDA ALEXANDER REMMY**
**Kwa kuwa Mdai/wadi ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba MADAI YA FEDHA TSH 21,650,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 20 mwezi 08 mwaka 2024 saa
2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 07 Mwezi 08 mwaka 2024

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**FOR DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 19558...... 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JUMA BISEKO MADHAHA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION PROBATE BY ESTA JOHN MADAHA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 18 Day of 09....................... 2024
Dated at Dodoma this 29 Day of July................2024

..........................................................................
PETITIONER

Presented for filing this 13..................day of 08...............2024

RESIDENT MAGISTRATE

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# WHO: Kufunga mpaka sio suluhu ya kudhibiti Mpox

**GENEVA, Uswisi**

MSEMAJI wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Tarik Jasarevic, amesema kufunga mipaka pekee haitakuwa suluhu ya kuzuia kusambaa kwa virusi vya homa ya nyani (Mpox).

Akizungumza na shirika moja la habari jana alisema uzoefu unaonyesha kuwa kufunga mipaka hakutavizuia virusi, akirejelea hatua kama hiyo ilipochukuliwa wakati wa janga la UVIKO-19.

Alisema kinachotakiwa kufanyika ni kuhakikisha waathirika wanatambuliwa ili wasiwaambukize wengine na kutoa wito wa upimaji wa mara kwa mara na watu kujichunguza ikiwa wana dalili za maambukizi ya mpox.

"Pia nitoe msisitizo kwa mataifa mbalimbali ulimwenguni kuimarisha zaidi mifumo yake ya kiafya katika kufuatilia maambukizi ya maradhi hayo," alisema Tarik.

Katika kuendeleza jitihada za kupambana na maradhi hayo, kampuni ya Denmark ya Bavarian Nordic ilisema inapanga kuongeza uzalishaji wa chanjo ya Mpox, pamoja na kufanya kazi na mashirika ya afya ya kimataifa ili kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa kinga hiyo.

Bavarian Nordic ilisema imekifahamisha kituo cha kudhibiti na kuzuia magonjwa barani Afrika (CDC) kwamba wanaweza kutengeneza dozi milioni 10 za chanjo ifikapo mwishoni mwa mwaka 2025, na kuwa wako tayari kuagiza barani humo hadi dozi milioni mbili mwaka huu.

"Tutatanua mtandao wetu wa uzalishaji na kulijumuisha bara la Afrika, pia tuko tayari kufanya kazi na Afrika CDC pamoja na WHO, ili kuwezesha chanjo hiyo kupatikana katika nchi zote," ilisema kampuni hiyo.

Pia Shirika la Afya la Umoja wa Ulaya limezitaka nchi wanachama wake zijiandae kwa uwezekano wa wagonjwa zaidi wa virusi vya homa ya nyani, hii ikiwa ni baada ya Sweden kutangaza mgonjwa wa kwanza mwenye virusi hivyo.

Kituo cha CDC kilisema takriban visa 18,737 vilivyothibitishwa kuwa ni vya maambukizi ya virusi vya Mpox vimeripotiwa barani Afrika tangu mwanzoni mwa mwaka huu, ikiwa ni pamoja na maambukizi 1,200 ndani ya muda wa wiki moja pekee.

"Kufikia sasa, visa 3,101 vya maambukizi yaliyothibitishwa na visa 15,636 vinavyoshukiwa vimeripotiwa katika nchi 12 wanachama wa Umoja wa Afrika (AU), na kusababisha vifo 541 hii ikiwa asilimia 2.89 ya kiwango cha vifo," ilisema sehemu ya taarifa ya CDC.

Kwa mujibu wa kituo hicho, visa zaidi vya maambukizi vimeripotiwa tangu mwanzo wa mwaka huu kuliko mwaka wote wa 2023, ulioshuhudia jumla ya visa 14,383.

Ilieleza kuwa nchi iliyoathirika zaidi na ugonjwa huo ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ambako aina mpya ya Clade 1b iligunduliwa kwa mara ya kwanza Septemba 2023, huku kukiwa na visa 1,005 (kati ya hivyo 222 vilithibitishwa, na 783 vinashukiwa) na jumla ya vifo 24 katika kipindi cha wiki moja.

Mikoa yote 26 nchini DRC, nyumbani kwa watu wapatao milioni 100, imeripoti visa vya homa ya nyani. Huku nchi jirani ya Burundi ikiripoti visa 173 ambavyo vinaashiria ongezeko la asilimia 75 katika wiki moja.

Idadi hiyo ya maambukizi inajumuisha aina tatu ya virusi vya homa ya nyani, ambavyo moja kati ya hizo ni kirusi kipya na hatari zaidi cha Clade 1b kinachoweza kuambukiza zaidi na kilichosababisha WHO kutangaza dharura ya afya ya kimataifa, ikiwa ni tahadhari ya juu zaidi ya shirika hilo.

***DW***



Picha ya mama na watoto wake wakiwa kwenye moja ya kambi wanazoishi watu waliokoseshwa makazi nchini Sudan. **PICHA: MTANDAO**

# Uingereza yaendelea kuiunga mkono Ukraine

**LONDON, Uingereza**

WAZIRI wa Ulinzi wa Uingereza, John Healey, amesema wataendelea kusimama karibu na Ukraine kwa muda wote itakavyokuwa, akieleza kuwa endapo Rais wa Russia, Vladimir Putin, atafanikiwa hataishia hapo, badala yake atasababisha wengine kama yeye kuwa na ujasiri.

Kiongozi huyo aliandika hayo jana katika gazeti la 'Sunday Express' ambamo aligusia operesheni ya Ukraine huko Kursk, kwenye eneo linalotambulika kuwa ni la Russia. Alisema baada ya wiki sita tu kama waziri wa ulinzi wa Uingereza, anaimani zaidi kuliko hapo awali kwamba ulinzi wa Uingereza na Ulaya unaanza Ukraine.

"Kwa mujibu huo, Uingereza imeungana katika kuunga mkono na tutasimama karibu na marafiki zetu shupavu wa Ukraine, uvamizi mkali wa wanajeshi uliofanywa Russia hivi karibuni ili kujilinda dhidi ya mashambulizi zaidi katika miji ya Ukraine, umefichua udhaifu wa jeshi la Russia na kuweka shinikizo kwa Putin," alisema.

Aliongeza kuwa chini ya Kifungu cha 51 cha Mkataba wa Umoja wa Mataifa (UN), Ukraine ina haki ya wazi ya kujilinda dhidi ya mashambulizi haramu ya Russia.

Aidha, alieleza kuwa ikiwa sheria ya kimataifa inazingatiwa, hiyo haizuii shughuli kwenye eneo la Russia huku akirejelea matumizi ya silaha za Waingereza nchini humo vikiwamo vifaru vilionekana katika eneo la Kursk.

"Tunapaswa kujivunia kwamba vifaa vilivyotolewa na Waingereza viko mikononi mwa Waukraine jasiri kwenye mstari wa mbele, zikiwasaidia kulinda silaha zao, nchi na kumweka Putin pembeni," alisema.

***BBC***

# Ubakaji watumika silaha ya vita Sudan

**KHARTOUM, Sudan**

UMOJA wa Mataifa (UN) umesema wanawake nchini Sudan wanakabiliwa na unyanyasaji wa kijinsia ikiwamo kufanyiwa vitendo vya ubakaji kama silaha ya vita wakati wakikimbia makazi yao baada ya wenza wao kupoteza maisha.

Taarifa ya UN iliyotolewa siku chache zilizopita ilisema pande zinazohusika katika vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Sudan tangu Aprili 2023 zimeshutumiwa kutumia unyanyasaji wa kijinsia na ubakaji kama silaha ya vita.

Mona Rishmawi, mjumbe wa jopo huru ya Umoja wa Kimataifa kuhusu ukweli na haki kuhusu Sudan, alitoa maoni yake kuhusu ripoti za unyanyasaji wa kingono dhidi ya wanawake nchini Sudan wakati wa mahojiano na Anadolu.

Rishmawi alisema kutokana na mzozo huo, wanawake wengi wamekuwa wakimbizi na wengi wamelazimika kusafiri kwenda nchi nyingine peke yao kwa sababu waume zao waliuawa.

"Wanawake wa Sudan mara kwa mara wamefurushwa na kukabiliwa na hatari mbalimbali wakati wa safari zao, kuna visa vingi vya watu kupotea. Wengi hawajui hatima ya wapendwa wao. Walihama mara nyingi ndani na nje," alisema.

Aliongeza kuwa familia mara nyingi huwa na watoto wengi, na wanawake huachwa kuwatunza peke yao, na kwamba wengi wao  wanalengwa na kuadhibiwa kutokana na majukumu yao katika jamii.

Pia alisema wanawake huficha unyanyasaji wa kijinsia ili kuepuka unyanyapaa. Huku vita nchini humo vikiendelea kwa zaidi ya miezi 15 sasa bila matumaini ya kupatikana upatanishi au usitishaji.

Mazungumzo ya amani yanayofadhiliwa na Marekani na Saudi Arabia yanafanyika mjini Geneva yanayohudhuriwa na wapiganaji wa jeshi la dharura RSF, japo upande wa jeshi la taifa umekataa kuhudhuria.

***TRT***

HABARI MICHEZO

# KMC FC yataka pointi sita Ligi Kuu nyumbani

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa KMC, John Matambala, amesema kikosi chake kimeiva kwenye maandalizi na kipo tayari kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara, huku ikihitaji kuanza kwa kukusanya pointi sita za nyumbani katika mechi zake mbili za mwanzo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kocha huyo alisema lengo lao ni kushinda michezo miwili ya mwanzo ambayo itacheza nyumbani dhidi ya Coastal Union na Azam FC na baada ya hapo wataendelea na mahesabu mengine.

"Sisi kama KMC tumejipanga kisawasawa, kila kitu kiko tayari, hivi sasa tunafanya maandalizi ya mwisho kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara, tunawasubiri hao Coastal Union watoke Angola waje tuanze nao.

"Tunafahamu ni timu nzuri, tumewaona wakicheza na Azam pamoja na Simba, tutakabiliana nao, tunawaheshimu wanacheza michezo ya kimataifa, lakini tutapambana, uzuri ni kwamba mechi mbili za kwanza tutacheza nyumbani kwanza kabla ya kutoka, hivyo tunatarajia kupambana ili kuzoa kwanza pointi sita," alisema kocha huyo.

KMC, ambayo inatumia uwanja wao wa nyumbani, KMC, Mwenge, Dar es Salaam, imepangwa kucheza dhidi ya Coastal Union, Agosti 29, mara baada ya kutoka Angola kucheza dhidi ya Bravos do Maqius, katika mchezo wa awali, Kombe la Shirikisho barani Afrika, mchezo mwingine utakuwa, Septemba 26, mwaka huu, dhidi ya Azam FC.

Kocha huyo anaamini kuwa maandalizi waliyoyafanya pamoja usajili wao, umekifanya kikosi chao kuwa imara zaidi ya kile cha msimu uliopita chini ya kocha raia wa Somalia, Abdihamid Moalin.

Wachezaji waliowasajili KMC kwa ajili ya msimu ujao ni Imasil Mpaki, Ajoh Austin, Oscar Paul, Nickson Kassam Mosha, Fabien Mutombora, Jean Nyezimana na Salum Athumani ,Stopper.'

# BONDIA CHANGALAWE ALIPA KISASI KWA KABEJI 'USIKU WA MABINGWA'

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA Yusuf Changalawe, ameshinda pambano lake la usiku wa kuamkia jana na kufuta uteja mbele ya Bingwa wa Afrika, Pita Kabeji kutoka DR Congo katika mapambano ya Usiku wa Mabingwa wa IBA yaliyofanyika kwenye ukumbi wa makumbusho wa Adwa jijini Addis Ababa, Ethiopia.

Pambano hilo lililokuwa na mvuto zaidi kati ya miamba hao wa Afrika katika uzani wa Light Heavyweight Kg 80, lilikuwa la tatu kukutana wakali hao huku Changalawe akipoteza mara mbili dhidi ya Kabeji katika hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Afrika Accra - Ghana 2023 na katika fainali ya mashindano ya Mandela Durban 2024.

Changalawe aliyecheza kwa ustadi wa hali ya juu na kutumia akili nyingi, alishinda kwa matokeo ya kutenganisha (split decision) katika pambano hilo la round nane (8) huku akishangiliwa zaidi na Waethiopia waliovutiwa na mchezo wake.

"Ninamshukuru Mungu kwa ushindi wa leo, nawashukuru IBA, AFBC na BFT kwa kunipa nafasi hii, hakika nimetimiza ndoto yangu kulipiza kisasa kwa Kabeji," alisema Changalawe.

Usiku wa Mabingwa wa IBA ni matamasha ya ngumi yanayozunguka duniani na hili la Addis Ababa likiwa la kwanza kufanyika katika Bara la Afrika, huku lengo kuu likiwa ni kuwajengea uwezo mabondia wa ridhaa kwenye ngumi za kulipwa pamoja na kuwainua kiuchumi.

Changalawe aliambatana na Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya ,Faru Weusi wa Ngorongoro', Samwel ,Batman' Kapungu, akisaidiana na Katibu Mkuu, Makore Mashaga.

"Tunashukuru kwa ushindi huu, tunaushukuru Ubalozi wa Tanzania nchini Ethiopia, Watanzania wote waishio Addis Ababa na wenyeji wa Ethiopia waliojitokeza kutuunga mkono na kutushangilia" alisema Raisi wa Shirikisho la Ngumi Tanzania, Lukelo Willilo.




Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa (kushoto), akimkabidhi Sh. milioni 20 za 'Goli la Mama', Rais wa Yanga, Hersi Said, kama zawadi ya ushindi kutoka kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kama utaratibu wake kwa klabu za Tanzania zitakazoshinda katika mechi zao za kimataifa. Yanga na Azam zinashiriki Ligi ya Mabingwa Afrika, wakati Simba na Coastal Union wakicheza Kombe la Shirikisho. Kila goli la ushindi Rais Samia ameahidi kutoa Sh. milioni tano na Yanga juzi ilishinda mabao 4-0 dhidi ya Vital'O ya Burundi katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA**

# Ngushi mfungaji bao la kwanza rekodi ikijirudia

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Mashujaa FC, Crispin Ngushi, ameweka rekodi ya kufunga bao la kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, ambapo kwa misimu minne imejirudia kuwa ni bao pekee linalozipa timu zao ushindi.

Ngushi, straika wa zamani wa Yanga, akiwa ndiyo kwanza amejiunga na Mashujaa FC akitokea Jangwani, alipachika bao pekee dakika ya 33, juzi kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika Kigoma, na kuipa timu yake ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji.

Bao hilo limemfanya kuwa mchezaji wa kwanza msimu huu kufunga baada ya timu za Pamba Jiji na Tanzania Prisons kushindwa kufungana katika mechi pekee ya ufunguzi ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024/25.

Alilifunga kwa mguu wa kulia, akiwa ndani ya eneo la hatari, akipenyezewa pasi kutoka kwa Hassan Ally.

Kwa misimu minne sasa, mabao ya wafungaji wa mwanzo wa msimu yamekuwa yakizipa ushindi wa bao 1-0 timu zao.

Ni msimu wa 2019/20, ndio haikuwa hivyo, kwani bao la kwanza lililofungwa na Paschal Liponda wa Mbao FC, ikicheza dhidi ya Alliance, Uwanja wa CCM Kirumba, Agosti 24, 2019, lilirudishwa na timu hizo kutoka sare ya bao 1-1.

Baada ya hapo msimu wa 2020/21, Birigimana Blaise, aliifungia la ufunguzi msimu huo, Spetemba 6, 2020, Uwanja wa Majaliwa, Rungwa, Lindi, Namungo ikiifunga Coastal bao 1-0, William Edger, akiifungia bao la kwanza la msimu, Uwanja wa Manungu Complex uliopo Turiani, Morogoro, Septemba 27, 2021, Mbeya Kwanza ikiichapa Mtibwa Sugar bao 1-0, 2021/22.

Ally Bilal wa Ruvu Shooting alifungua msimu wa 2022/23 kwa bao lililoipa ushindi wa 1-0 Ruvu Shooting dhidi ya Ihefu, Agosti 15, 2022, Uwanja wa Highland Estates, Mbarali mkoani Mbeya, na uwanja huo huo msimu uliofuata, 2023/24 bao la kwanza la msimu lilifungwa hapo hapo na Elius Maguli, Geita Gold ikishinda 1-0 dhidi ya Ihefu, Agosti 15, mwaka jana.

Kipigo cha bao hilo juzi, kinaifanya Dodoma Jiji kuendeleza uteja, kwani katika mechi ya mwisho ya kufunga dimba msimu uliopita, Mei 28, mwaka huu, ilibugizwa mabao 3-0, na kuiwezesha Mashujaa kubaki Ligi Kuu, huku Dodoma ikiponea chupuchupu kwa msaada wa Simba kuifunga JKT Tanzania na kuipeleka kucheza ,play off'.

## ZISIKUPITE

### ERIKSEN RUKSA KUONDOKA

MANCHESTER United imemwambia kiungo wa Kimataifa wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 32, kwamba yuko huru kutafuta klabu mpya mwezi huu na anaweza kuondoka kwa mkataba wa bei nafuu. ***(Football Insider)***

### UNITED YAMPOTEZEA DE JONG

KLABU ya Manchester United haina mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong, 27. ***(Metro)***

### FELIX, GALLAGHER KUPISHANA

ATLETICO Madrid inalenga kukamilisha mauzo ya mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 24, kwa Chelsea na kumsajili kiungo wa kati wa ,The Blues' hao, Conor Gallagher (24), ifikapo Jumatano wiki hii. ***(AS)***

### FOFAFA HUYOOO MILAN

AC Milan imefikia makubaliano na Monaco kwa ajili ya kiungo wa kati wa Ufaransa, Youssouf Fofana mwenye umri wa miaka 25, ambaye pia ananyatiwa na Manchester United. ***(Anga Italia)***

### BERGE RASMI AJADILIWA

MANCHESTER United inaendelea kujadiliana na Burnley kuhusu mkataba wa kiungo wa Norway, Sander Berge, 26. ***(Sky Sports)***

### JOHNSTON SASA AGOMBEWA

KLABU za Stoke City, Swansea City na Oxford United zina nia ya kumsajili beki wa Scotland, Max Johnston mwenye umri wa miaka 20 kutoka Sturm Graz. ***(Football Insider)***

### ARCHER ATAJWA KWA MKOPO

UNION Berlin na Getafe zinaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa England na Aston Villa, Cameron Archer, 22. ***(Fabrizio Romano)***

### MADUEKE SOKONI MILIONI SITA

CHELSEA imeweka bei ya pauni milioni sita kwa klabu yoyote inayotaka kumsajili winga wa England, Noni Madueke, 22. ***(Athletic)***

### ALONZO AITAKA UNITED

MLINZI wa zamani wa Chelsea na Hispania, Marcos Alonso mwenye umri wa miaka 34, angependa kujiunga na Manchester United baada ya kuwa mchezaji huru anapoondoka Barcelona. ***(Fabrizio Romano via Givemesport)***

### DOUE ATAKIWA PSG

PARIS St-Germain iko tayari kuipiku Chelsea katika mbio za kumsajili kiungo wa Klabu ya Rennes ya Ufaransa chini ya umri wa miaka 23, Desire Doue. ***(ESPN)***

### BOSCAGLI NA BRIGHTON

KLABU ya Brighton imewasilisha ofa iliyoboreshwa kwa mlinzi, Olivier Boscagli mwenye umri wa miaka 26, ambaye aliichezea timu ya vijana ya Ufaransa, lakini bado inaonekana kutoafikiwa na PSV Eindhoven. ***(Voetbal International)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA AKIONA KIVULI CHA MESSI KWA SAKA

●●●Kwa wachezaji wazuri ni hivyo, lakini yeye hufanya hivyo wakati wote...

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amekiri aliona vivuli vya Lionel Messi katika bao la Bukayo Saka dhidi ya Wolverhampton Wanderers.

Baada ya kutoa pasi ya bao la kufutia machozi la Kai Havertz, Saka alifunga bao lake baada ya mapumziko, akikata kutoka wingi ya kulia na kuachia shuti kali ambalo lilimshinda kipa Jose Sa na kujaa wavuni.

Ingawa kuonekana kwa Saka akikata ndani ya mguu wake wa kushoto si jambo geni, Arteta alisisitiza kutokuwa na uwezo wa mabeki kumzuia kunakumbusha ubora wa Messi kwenye mpira.

"Kwa wachezaji wazuri ni hivyo, na Messi najua atakuja hapa na kuweka mpira hapo," alisema Arteta. "Lakini yeye hufanya hivyo wakati wote. Huwezi kumzuia. Huo ndio ubora wa mchezaji."

Arteta aliendelea kukiri kuwa alifikiria kumuacha Saka katika kikosi cha kwanza cha Arsenal baada ya msimu wake mfupi wa kujiandaa na msimu mpya, lakini pamoja na Declan Rice na David Raya, walimkuta winga huyo akiwa amedhamiria kuichezea klabu yake.

"Lazima uelewe kweli walipo, wanachohitaji, ili kuwapa nafasi na wapumue," Arteta alisema kuhusu watatu hao. „Walipitia mengi na watoto hao wamecheza mpira mwingi katika miaka miwili iliyopita.


"Lakini unapoona utayari huo, nguvu ya kusema ,nimefurahi sana kurudi' na unaona hiyo ni kweli, ni ishara nzuri.

„Sishangai. Hayo ni mawazo yao. Mara baada ya [mwisho], walisema ,nitakuwa tayari kwa mchezo wa kwanza'.

"Nilizungumza nao majira ya joto ili kujaribu kupanga mpango wao bora. Walitaka kuwa mapema, walitaka kurejea. Tayari walikuwa wanajiandaa. Haya ndiyo mawazo tunayoyahitaji. Ikiwa wachezaji wanafanya hivyo, basi maelewano yatakuwa karibu na timu na watapanda kiwango hicho ndicho tunachohitaji."

HABARI MICHEZO

# FLICK AMTAKA GUNDOGAN KUBAKI BARCA



**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick amesema amezungumza na Ilkay Gundogan na kwamba anadhani atasalia katika klabu hiyo licha ya kutocheza mechi ya kwanza ya LaLiga dhidi ya Valencia Jumamosi.

Gundogan hakusafiri na kikosi kama "tahadhari" baada ya kugonga kichwa chake dhidi ya Monaco mapema wiki iliyopita.

Lakini ripoti katika vyombo vya habari vya ndani zilidai Gundogan, ambaye alijiunga tu kutoka Manchester City msimu uliopita wa majira ya joto, ameomba kuondoka kabla ya dirisha la usajili kufungwa mwezi huu.

"Jumatatu, alikuwa na jeraha [kichwani] na shida kadhaa, kwa hivyo tulichukua uamuzi wa kumuacha nyumbani," Flick alisema katika mkutano na waandishi wa habari alipoulizwa kuweka wazi hali hiyo baada ya timu yake kuanza msimu, kwa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mestalla.

"Nilizungumza naye [wiki hii], ni kweli, ndiyo. Nilizungumza ili kujua tu jinsi anavyohisi. Ninamfahamu vizuri sana. Ninathamini ni mchezaji wa aina gani na pia kama mtu.

"Tulizungumza kuhusu kila kitu. Si kwako [kujua], ni kwa ajili yetu tu. Nina hisia kwamba atasalia."

Vyanzo vilivyo karibu na Gundogan vilikariri msimamo huo kwa ESPN, vikisema Mjerumani huyo anatarajia kubaki Barca na kwamba alikosa mchezo wa Valencia baada ya kuumwa na kichwa na kizunguzungu alipokuwa mazoezini.

Bila Gundogan, timu changa ya Barca ilianza kampeni mpya kwa ushindi, huku Robert Lewandowski akifunga mara mbili walipokuwa nyuma baada ya Valencia kuchukua uongozi kupitia Hugo Duro.

Huku Gavi na Frenkie de Jong pia wakiwa wamejeruhiwa, na Pedri anafaa kwa benchi pekee, Flick aliwapanga wachezaji wawili wa kiungo Marc Bernal (17), na Marc Casado (20). Beki Pau Cubarsí na winga Lamine Yamal walikamilisha wachezaji watatu wa umri wa miaka 17 katika safu ya kuanza.

"Si mtihani, ilikuwa mechi muhimu sana kwetu," Flick aliongeza alipoulizwa kuhusu matumizi yake ya vijana wengi.

"Preseason haikuwa rahisi sana, kwa wachezaji waliorejea kutoka Euro na Olimpiki, na niseme wachezaji wachanga kutoka La Masia walifanya vizuri kabla ya msimu mpya na leo. Wiki sita tunafanya nao mazoezi na wanaimarika sana na wanastahili leo kucheza.

"Ni vema kuwa na wachezaji hawa hapa wenye ubora huu. Tunaweza kuona leo kile wachezaji wanachofanya. Ni nzuri sana. Inatusaidia sana."

## Greenwood gari limewaka Ufaransa

**MARSEILLE,** Ufaransa

MASON Greenwood amefunga mabao mawili katika mechi yake ya kwanza akiwa na Marseille katika ushindi wa 5-1 dhidi ya Brest kwenye mchezo wao wa ufunguzi wa Ligi Kuu Ufaransa Jumamosi.

Greenwood, fowadi wa zamani wa Manchester United ambaye alihamia Marseille msimu huu wa majira ya joto, alihusika katika mabao yote matano kwani pia alitoa pasi mbili za mabao na kuzalisha penalti ambayo Elye Wahi alifunga.

Mechi ya kwanza ya Greenwood ya Ligue 1 ilipokelewa kwa shangwe ambazo zilisikika katika uwanja wote wa Brest wa Francis-Le Ble kila alipogusa mpira.

Fowadi huyo mwenye umri wa miaka 22, alikamatwa mwaka wa 2022 na baadaye kushtakiwa kwa jaribio la ubakaji, kudhibiti na kulazimisha tabia na kushambulia. Kesi hiyo ilitupiliwa mbali mwaka jana.

Brest, ambao walimaliza wa tatu msimu uliopita na wanatarajiwa kushiriki Ligi ya Mabingwa, walitatizika muda wote wa mechi. Penati iliyokosa na Romain Del Castillo katika kipindi cha kwanza ilionyesha ukosefu wao wa usahihi.

"Hiki hakikuwa kiwango chetu," Kocha Mkuu wa Brest, Eric Roy, alisema. "Tuliwapa nafasi nyingi kwenye safu ya ulinzi."

Baada ya ushindi wa PSG wa mabao 4-1 dhidi ya Le Havre katika mechi ya ufunguzi wa msimu Ijumaa iliyopita, Marseille wanaongoza kwenye msimamo kwa tofauti ya mabao baada ya mechi ya kwanza ya kocha Roberto de Zerbi kuongoza.




## Ronaldo bado sana kubeba taji Saudia

**RIYADH,** Saudi Arabia

CRISTIANO Ronaldo bado anasubiri kombe lake la kwanza la ndani nchini Saudi Arabia baada ya Al Nassr kufungwa mabao 4-1 na Al Hilal kwenye michuano ya Saudi Super Cup Jumamosi.

Mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or, alifunga bao la kwanza kabla ya muda wa mapumziko katika mechi ya ufunguzi wa pazia la msimu kati ya mabingwa wa Saudi Pro League, Al Hilal na washindi wa pili Al Nassr.

Hata hivyo, fowadi huyo mwenye umri wa miaka 39, baadaye alivurugwa baada ya Al Hilal kufunga mabao manne katika muda wa dakika 17 katika kipindi cha pili.

Ronaldo alijiunga na Al Nassr Desemba 2022 na kuweka rekodi ya ligi msimu uliopita akiwa amefunga mabao 35.

HABARI MICHEZO

# COASTAL YATAJA KILICHOWASIBU KIPIGO MICHUANO CAF ANGOLA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kukung'utwa mabao 3-0 ugenini dhidi ya Bravos do Maquis ya Angola, wachezaji wa Coastal Union wamesema hali ya hewa iliwaathiri kwa kiasi kikubwa katika mchezo huo.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Gerald Gwalala, alisema hali ya baridi nchini Angola ilichangia kwa kiasi kikubwa, lakini pia matumizi ya nguvu kwa wapinzani wao pia lilikuwa tatizo kwao.

"Mchezo ulikuwa mgumu upande wetu, baadhi ya vitu vilituathiri, kwanza ni hali ya hewa, lakini wenzetu walikuwa wakicheza soka la kutumia mabavu zaidi, ila benchi la ufundi limeona, mpira ni mchezo wa makosa, tumefanya makosa wametuadhibu, naamini makocha watatupa maelekezo kuelekea mechi ya pili nyumbani, mchezo haujaisha mpaka marudiano," alisema Gwalala.

Ulikuwa ni mchezo wa Kombe la Shirikisho barani Afrika, uliopigwa juzi Uwanja wa Nacional da Tundavala nchini Angola, ukiwa ni wa kwanza wa kimataifa kwa wawakilishi hao wa Tanzania baada ya miaka 35. Mara ya mwisho kwa timu hiyo kucheza mechi za kimataifa ilikuwa ni 1989, baada ya kutwaa Ubingwa wa Tanzania Bara 1988.

Yalikuwa ni mabao ya Joaquim Cristovao Paciencia dakika ya 22 na 45 na Luis Manico Goncalves dakika ya 81, yaliyoiweka Coastal kwenye wakati mgumu kwa kusonga mbele kwenye hatua ya raundi ya kwanza ya michuano hiyo, ambapo sasa italazimika kushinda kuanzia mabao 4-0 katika mchezo wa marudiano utakaopigwa, Agosti 25, mwaka huu Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Kocha Mkuu, David Ouma, alionyesha kusikitishwa na timu yake kuruhusu mabao rahisi, mawili yakiwa ya aina moja.

"Dakika 15 za mwanzo tulicheza vema, lakini baadaye tukapotea, tumefungwa mabao ya aina moja, tumeruhusu mabao rahisi sana," aliongea kocha huyo kwa masikitiko.

KONDE...




Bondia Mtanzania Yusuf Changalawe (kulia), akimtupia konde mpinzani wake, Pita Kabeji wa DR Congo, katika pambano la Usiku wa Mabingwa wa IBA, lililofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia juzi. Katika pambano hilo la raundi nane, Changalawe alishinda kwa matokeo ya kutenganisha (split decision). **HABARI UK. 20. PICHA: MPIGAPICHA**

# Simba Queens kibaruani Ethiopia

**Na Somoe Ng'itu**

WAWAKILISHI wa Tanzania Bara, Simba Queens wanatarajia kuanza kampeni ya kuwania ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), kwa kuvaana na FAD ya Djibouti katika mechi ya Kundi B itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Abebe Bikila jijini Addis Ababa, Ethiopia.

Simba Queens ilipata tiketi ya kushiriki mashindano hayo baada ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), msimu uliomalizika wa 2023/2024.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Juma Mgunda, aliliambia gazeti hili kikosi chake kimejiandaa vema kuelekea mchezo huo na anaamini wataanza vizuri mashindano hayo.

Mgunda alisema kila mechi kwao ni sawa na fainali, hivyo wamejipanga kupambana na hawatawadharau wapinzani wao. "Tuko tayari kwa ajili ya mechi ya kesho (leo), kila mchezaji anajua anachotakiwa kukifanya, ninaamini tutapata matokeo mazuri katika safari ya kuwania taji hili," Mgunda alisema.

Simba Queens itashuka tena uwanjani kucheza mchezo wake wa pili Jumatano dhidi ya Kawempe Muslim na itamaliza mechi za hatua ya makundi Agosti 23, mwaka huu, kwa kuwakabili mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Burundi, PVB Buyenzi.

Timu mbili zitakazomaliza katika nafasi mbili za juu zitatinga hatua ya nusu fainali na fainali ya mashindano hayo zitafanyika Agosti 31, mwaka huu.

Wakati huo huo, wenyeji wa michuano hiyo, CBE walianza vema mashindano hayo juzi kwa kupata ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Rayon Sports Women FC ya Rwanda katika mechi ya ufunguzi iliyochezwa.

## Awesu, Mashaka moto mpya Simba

INATOKA UK. 24

geisha kwa mabao 2-0, kiungo mshambuliaji aliyesajiliwa msimu huu kutoka KMC, Awessu, alipachika bao la tatu kwa mpira aliopiga kwa ufundi wa hali ya juu.

Akiwa pembeni kidogo ndani ya eneo la hatari, aliupiga mpira ambao ulionekana kama unaelekea nje, lakini ulikatika na kugonga nguzo ya chini upande wa kulia kwa kipa Haroun Mandanda na kujaa wavuni.

Msimu uliopita Simba ilichukua pointi zote sita kwa Tabora United, ikiifunga mabao 4-0, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Februari 6, na mechi ya mzunguko wa pili, ikashinda mabao 2-0, mchezo uliochezwa Mei 6, mwaka huu katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

## Gamondi: Vital'O wameijua Yanga

INATOKA UK. 24

wa na wachezaji wapya, Prince Dube aliyesajiliwa kutoka Azam FC na Clatous Chama aliyetokea Simba, pamoja na mengine ya Clement Mzize na Stephane Aziz Ki yaliyoipa ushindi wa idadi hiyo ya mabao.

Matokeo hayo yanaifanya Yanga kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kucheza raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya mshindi kati ya CBE ya Ethiopia na SC Villa ya Uganda.

Katika mechi yao iliyochezwa juzi, Uwanja wa Mandela, Uganda, CBE ilishinda ugenini mabao 2-1.

Yanga iliyokuwa inacheza ugenini kikanuni katika mchezo wa juzi, kutokana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), kuvifungia viwanja vya Burudi kutokana na kukosa sifa, itarudiana na Vital'O, Agosti 24, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, ambapo sasa itakuwa ipo nyumbani.

Kwa upande wa Vital'O, Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Selemani Hamisi, alisema Yanga ilionesha uwezo mkubwa katika mchezo huo.

"Hatukutarajia kufungwa magoli mengi kama haya kutokana na maandalizi ambayo tuliyafanya kipindi chote ambacho tulikuwa kambini," alisema Hamisi.

Alisema licha ya kupoteza bado hawajakata tamaa na badala yake wanakwenda kujipanga upya kwa ajili ya mchezo wao wa marudiano.

Hamisi alisema anaipongeza Yanga kutokana na uwezo iliouonesha na kwamba anaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano na mapokezi waliyowapa tangu waingie hapa nchini.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sahabo Parris, alisema hajaridhishwa na matokeo waliyoyapata na kuahidi kwenda kuyafanyia kazi makosa yaliyojitokeza ili yasijirudie kwenye mchezo wao ujao.

"Ninakwenda kuyafanyia kazi makosa ambayo nimeyaona katika mchezo huu ili yasijitokeze katika mchezo wetu wa marudiano," alisema Parris.

Michezo
Jumatatu Agosti 19, 2024
Nipashe

## Arteta akiona kivuli cha Messi kwa Saka

UKURASA 21



# Awesu, Mashaka ni moto mpya Simba

**●●●Waiamsha Simba ikiirarua Tabora United huku Che Malone naye akifanya yake kwa...**




Kiungo Mshambuliaji wa Simba, Awesu Awesu, akiachia shuti kali lililozaa bao la tatu kwa Simba wakati ikishinda 3-0 dhidi ya Tabora United kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa jana katika Uwanja wa KMC uliopo Mwenge, Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili ya wachezaji wapya, Valentino Mashaka na Awesu Awesu, pamoja na lingine lililofungwa na Fondoh Che Malone, yaliiwezesha Simba jana kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Tabora United, ikiendeleza rekodi yake ya kutopoteza mechi yoyote ya mzunguko wa kwanza kwa misimu 17.

Mara ya mwisho Simba kupoteza mechi ya kwanza ya Ligi Kuu, ilikuwa ni Septemba 23, 2007, Ligi Kuu msimu wa 2007/08, kwenye Uwanja wa Mkwakwani, ilipochapwa bao 1-0, dhidi ya Coastal Union likiwekwa wavuni na Sunday Peter.

Misimu yote 17 iliyosalia Simba haijawahi kupoteza zaidi ya kushinda na kutoka sare.

Beki wa kati raia wa Cameroon, ameingia kwenye rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga bao la msimu kwenye kikosi cha Simba, alipofanya hivyo dakika ya 13 ya mchezo huo uliopigwa, Uwanja wa KMC uliopo Mwenge, Dar es Salaam.

Malone aliipatia Simba bao baada ya kuruka juu zaidi ya wachezaji wote na kuunganisha kwa kichwa mpira wa kona fupi iliyopigwa na Jean Charles Ahoua.

Bao hilo lilifungwa baada ya kona mbili kupigwa, ya kwanza ikipigwa na Balua, ikaokolewa na Salum Chukwu, ya pili ikipigwa na Joshua Mutale, ambaye alipiga fupi kwa Ahoua, aliyeuinua langoni na kumkuta mfungaji.

Tabora United walianza mechi kwa kuwaachia Simba, wao wakikaa nyuma ya mpira kwa muda mrefu huku wakifanya mashambulizi ya kushtukiza mara chache, na hata hivyo hayakuwapa tabu sana mabeki na kipa wake Moussa Camara.

Simba ingeweza kuandika bao dakika ya tano kupitia kwa Steven Mukwala, lakini aliunganisha vibaya krosi ya Edwin Balua.

Baada ya bao hilo, Simba iliendelea kulisakama lango la Tabora United, lakini tatizo sugu la ukosaji wa mabao liliendelea kuwaandama. Kuna wakati wachezaji wenyewe kwa wenyewe walionekana kukosa mawasiliano, huku pia ikionekana kila mmoja anataka kufunga licha ya kuwa kwenye eneo gumu.

Shuti la Ahoua, liligonga mwamba dakika ya 25 alipounganisha krosi fupi kutoka kwa Mutale, ambaye dakika chache baadaye aliumia na nafasi yake kuchukuliwa na Awessu.

Kipindi cha pili, Kocha Mkuu, Fadlu Davis, alilazimika kufanya mabadiliko ya kuwatoa kwanza Ahoua, Mukwala, Mzamiru Yassin na Shomari Kapombe, nafasi zao zikachukuliwa na Valentino, Kibu Denis, Agustine Okejepha na Kelvin Kijili, mabadiliko ambayo yaliisaidia kupata mabao mawili kipindi hicho.

Alikuwa ni straika aliyesajiliwa kutoka Geita Gold, Valentino, aliyepachika bao la pili likifungwa mara nyingine kwa kichwa.

Aliruka juu kuunganisha krosi iliyopigwa na nahodha, Mohamed Hussein ,Tshabalala.

Wakati kila mmoja akidhani mechi hiyo in-

INAENDELEA UK. 23

# Gamondi: Vital'O wameijua Yanga

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema alikerwa na maneno ya Ofisa Habari wa Vital'O ya Burundi, Arsene Buccuti, ambaye alionesha dharau kubwa kwa timu yake, hivyo kipigo cha mabao 4-0 ilichokipata ni ujumbe tosha kumwambia „hiyo ndiyo Yanga, na sasa umejua kuwa ni timu ya aina gani".

Akizungumza baada ya mchezo wa hatua ya awali, Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya timu hiyo ya Burundi uliochezwa juzi, Uwanja wa Azam Complex, Gamondi alitaka mpira wa miguu uheshimiwe kwa sababu watu wanaongea sana kuhusu timu yake na wengine wakionekana kuibeza, lakini yeye anawajibu uwanjani tu.

"Mpira ni lazima uheshimiwe, kuna timu zinaongea sana, kwa hiyo tumewaonesha kuwa sisi ni Yanga, wametambua kuwa ni timu kubwa na sasa baada ya kipigo hiki wanaijua Yanga," alitamba Gamondi.

Kabla ya mchezo huo, Buccuti, alitamba kuwashikisha adabu Yanga, akidai haiogopi, na si tishio kama watu wanavyoizungumza.

"Wengi wanatuona kama wepesi tu, kwa sababu tumecheza na Pamba Jiji tumetoka sare tena tumesawazisha bao mwishoni, lakini hawajui kuwa kila mechi ina mbinu zake, wachezaji wa Pamba ni wazuri, pia hatuwajui kwa sababu hatujawahi kuona video zao, lakini Yanga tunaziona na tunazifanyia kazi, hatutishwi na mchezaji yeyote.

„Nasikia wanasema tu watatufunga mabao matatu mpaka manane, mpira hauchezwi mdomoni, unachezwa uwanjani ndani ya dakika 90, sisi tumekuja, tumejipanga na kumejidhatiti, nasema hatujatoka bure huko Burundi, tutawashangaza," alisema Buccuti kabla ya mechi hiyo, maneno ambayo yalimkera Gamondi.

Akizungumzia mchezo huo, Gamondi alisema kipindi cha kwanza walitengeneza nafasi nyingi, lakini hawakuzitumia, hivyo akaamua kubadilisha mbinu kipindi cha pili.

"Tuna kikosi kizuri, lengo lilikuwa ni kushinda mechi hii, kipindi cha kwanza ilikuwa twende mapumziko na mabao matatu, tumekosa mabao ya wazi.

„Kipindi cha pili nikawaambia wachezaji wangu kuwa tunapaswa kuongeza kasi, na nikabadilisha mfumo wa uchezaji, na kweli tumecheza vizuri na tukatengeneza nafasi nyingi na kuzitumia," alisema raia huyo wa Agrentina.

Yalikuwa ni mabao mawili yaliyofung-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >